AMBOLA

SEASON 01

PALE MASHUJAA
WANAPOLISALITI TAIFA LAO

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

HADITHI HII NI YA KUBUNI HAINA MAHUSIANO NA TUKIO LOLOTE LA KWELI.

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

SIMULIZI ZA MAPENZI

1.MISS TANZANIA
2.SERENA
3.BEFORE I DIE
4.BEYOND PAIN

SIMULIZI ZA UPELELEZI

5.PENIELA
6.QUEEN MONICA
7.THE FOOTBALL
8.I DIED TO SAVE PRESIDENT
9.KIAPO CHA JASUSI
10.KIKOSI CHA SIRI
11.SIRI
12.SCANDAL(KASHFA)
13.CAPTURE OR KILL MISSION
14.JAMII YA SIRI

MAWASILIANO

0764294499

© 2020 Masimulizi.Haki zote zimehifadhiwa

DAR ES SALAAM – TANZANIA

“Nchi zote duniani zinaongozwa na watu.Mimi niliwahi kupata heshima ya kuongoza nchi hii,sasa leo Rais Mwinyi aniongoza.Hivi sasa tunazungumza kuona nani anafaa kutusaidia kuongoza.Nchi zinaongozwa na watu,kumbe zitaongozwa na nani? Hatuna malaika,hatuna nini,ndivyo alivyotaka Mwenyezi Mungu nchi hizi tuziongoze wenyewe sisi hawa hawa.Lakini haziongozwi kutokana na

akili ya mtu,zinaongozwa na katiba na sheria.Ni kweli nchi zinongozwa na watu lakini hao watu wanaongozwa na sheria.Haiwezekani mtu mtu anapata ushauri kutoka kwa mkewe halafu kesho tunakuta jambo limetokea"(Kicheko kikubwa kutoka kwa waandishi wa habari.)

Mathew Mulumbi aliyekuwa katika chumba cha mapumziko akitazama hotuba ya baba wa taifa aliyoitoa mwaka 1995 alipozungumza na waandishi wa habari, naye aliangua kicheko halafu

akaendelea kusikiliza kile alichokisema baba wa taifa

“Serikali corrupt popote hazikusanyi kodi. Serikali corrupt inachumwa na wenye mali.Inawafanyia kazi wenye mali .Serikali corrupt haikusanyi kodi!.Itabaki kufukuzana na vitu vidogo vidogo barabarani.Mkiwa corrupt mtaabudu wenye mali.Mimi ni mkristu,sijui Quran inasemaje lakini kwa maneno ya Yesu kristu huwezi kutumikia mabwana wawili.Moja fedha lingine

Mungu.Utachagua katika wawili hao.”

Mara Mathew alishtuliwa na sauti laini nyuma yake.

“Wewe utachagua yupi katika hao mabwana wawili?

Mathew aligeuza shingo akakutana na sura yenye tabasamu ya Latoya ambaye alimfuata pale sofani akambusu.

“Umeshindaje mpenzi wangu? Latoya aliuliza.

“Nimeshinda salama kabisa. Wewe umeshindaje? aliuliza Mathew

“Mimi pia nimeshinda salama”alijibu Latoya

“Nimewahi sana kurejea nyumbani ili nipumzike, ninahisi uchovu mwingi” alisema Mathew

“Pole mpenzi wangu.Tafadhali jipe muda wa kupumzika” alisema Latoya

“Ndiyo maana nimeamua kukutuma wewe uende Dubai ili na mimi nipumzike. Vipi

maandalizi ya safari yamekamilika? Mathew aliuliza

“ Maandalizi yamekamilika.Kesho ninaondoka” alijibu Latoya halafu kikapia kimya cha sekunde chache.

“Nilikuuliza swali bado hujanijibu.Wewe utachagua nini kati ya Mungu na fedha? Aliuliza Latoya.Mathew alicheka kidogo halafu alisema

“Ninamchagua Mungu. Yeye ndiye atupaye uhai na nguvu za kufanya kazi ili

kuitafuta fedha.Baada ya kuipata hiyo fedha tunaigawa mafungu.Fungu moja tunalirejesha kwake kama shukrani kwa kutoa sadaka,zaka n.k.Fungu lingine tunampa Kaisari yaani tunalipa kodi ili taifa lisonge mbele.”alijibu Mathew.Latoya alitabasamu halafu alisema

“Hii ni mara ya tatu ninakuona unaitazama hotuba hii ya baba wa taifa.Kulikoni? Hujaielewa mpaka sasa? Aliuliza Latoya

“Nimeielewa vizuri sana ila ninajikuta ninataka kuisikiliza tena na tena.Katika hotuba hii baba wa taifa alizungumza mambo makubwa kuhusu taifa letu.Aliitoa hotuba hii wakati wa kumtafuta rais wa tatu wa Tanzania lakini uzito wa yale aliyoyasema unaifanya hotuba hii iendelee kusikilizwa na vizazi kwa vizazi.Tunapoelekea katika uchaguzi mkuu wa Rais na wabunge ni vyema sana kuisikiliza hotuba hii ambayo ninaweza kusema ni wosia wa baba wa Taifa kwetu kuhusu rais wa namna gani anayefaa

kutuongoza.Hii ni sababu kila nipatapo wasaa ninautumia kujikumbusha maneno mazito ya baba wa taifa” alisema Mathew

“Unauonaje uchaguzi wa mwaka huu? Latoya aliuliza

“Ni uchaguzi wa kawaida kama chaguzi zilizopita.”Mathew alijibu

“Umekwisha jua nani utampa kura yako ya urais? Latoya aliuliza

“Kabla ya kufanya maamuzi ya nani nimpe kura

yangu ni lazima kwanza niwasikilize wagombea wote nifahamu sera zao.Lazima nifahamu nini watatufanyia pale tutakapowachagua.Wapo ambao wanakuja na sera nzuri sana lakini lazima nifahamu namna watakavyoweza kutekeleza sera hizo.Katika hizi chaguzi wapo wale ambao wana nia ya kweli ya kuwaletea maendeleo wananchi.Wapo wengine wanatafuta uongozi kwa ajili ya manufaa yao binafsi.Wapo pia wanaotumwa wagombee na wakubwa huko nje ili wakipata uongozi basi

iwe ni neema kwa wakubwa hao waliowatuma.Katika kapu la wagombea wako wa kila aina ndiyo maana kuna ulazima wa kuwafahamu nani ni nani.” Alisema Mathew

“Mathew kwa nini usigombee nafasi yoyote ya uongozi?Unafaa sana kuwa kiongozi.Ninakuhakikishia utakuwa kiongozi mzuri sana” alisema Latoya

“Wewe si wa kwanza kuniambia jambo hilo, lakini jambo hilo halipo hata kabisa

katika mawazo yangu” alijibu Mathew

“Kwa nini Mathew?

“Siwezi kuwa kiongozi mzuri.Nina hasira sana hasa na wale wanaochezea rasilimali za nchi hivyo naweza kujikuta nimefanya jambo ambalo kiongozwi hapaswi kulifanya.Nitabaki mwananchi mzalendo kwa nchi yangu.Nitalipa kodi zote ninazostahili.Nitatumia uwezo wangu wa kifedha kuhakikisha ninatengeneza ajira nyingi kwa wenzangu.”alijibu Mathew

“Mathew wewe ni mtu mwenye macho sita.Jambo ambalo sisi wengine tunaliona la kawaida lakini kwako unaweza ukalitazama na kugundua tatizo.Nataka kufahamu unauonaje uchaguzi mkuu mwaka huu? Kuna tatizo lolote linaweza kutokea? Aliuliza Latoya

“Umeniuliza swali gumu lakini mpaka sasa hakuna viashiria vyovyote vya kutokea matatizo katika uchaguzi wetu ingawa hatuwezi kujihakikishia kuwa tuko salama kwa sababu Tanzania

ni nchi inayomezewa mate na mabeberu kutokana na utajiri wake hivyo watataka kujua nani anashinda uchaguzi na hata kujaribu kufanya jitihada ili mtu wanayemtaka wao ashinde uchaguzi huu.Hata hivyo vyombo vya usalama viko macho usiku na mchana kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na salama.” Alijibu Mathew

“Ahsante sana kwa kunitoa hofu.Nimekuuliza swali hilo kwa sababu nchi nyingi za Afrika zimejikuta katika machafuko makubwa na

chanzo kikiwa uchaguzi mkuu.” Alisema Latoya

“Hilo unalosema ni kweli kabisa.Migogoro mingi si kwa nchi za Afrika pekee bali sehemu mbali mbali duniani imeanzia wakati wa uchaguzi.Walioko madarakani hawataki kutoka hivyo wanajitahidi hata kutumia mbinu chafu kuhakikisha wanaibuka washindi.Wale wanaotaka kuingia madarakani nao hawakubali kushindwa na machafuko huanzia hapo.Kwa upande wa bara letu la Afrika,machafuko

mengi yanayotokea wakati wa uchaguzi yana mkono wake kutoka nje ya bara hili.Kwa hapa Tanzania tumepiga hatua kubwa kwani uchgauzi mkuu tunauendesha kwa fedha zetu za ndani.Kutegemea mataifa makubwa ya nje kugharamia chaguzi zetu ni hatari sana na hicho kinazigharimu nchi nyingi za bara hili." Mathew alikatishwa na Latoya

"Tuachane na hayo ya siasa.Vipi kuhusu sherehe ya kesho maandalizi yamekamilika? Latoya aliuliza

“Nimezunguza na Gosu Gosu maandalizi yamekamilika” alijibu Mathew

“Nilitamani sana kuwepo katika hiyo sherehe lakini safari hii nayo ni muhimu sana” alisema Latoya

“Usijali mimi nipo nitakuwakilisha kama wewe unavyokwenda kuniwakilisha Dubai.Sehemu zote mbili ni muhimu kwetu hivyo lazima tugawane majukumu” Alisema Mathew

“Unawaonaje Ambola na Gosu Gosu? Latoya aliuliza

“Sioni tatizo lolote kwao.Wanapendana sana.Nina uhakika mapenzi yao yatakwenda mbali.Ninampongeza Gosu Gosu kwa kuamua kutulia na huyu mpenzi wake wa sasa.Alikuwa mtu wa kuruka ruka hovyo lakini baada ya kumpata Ambola ametulia kabisa.” Alisema Mathew.Kilipita kimya kifupi halafu Latoya alisema

“Mathew,mpaka leo ninaona kama ndoto mimi kuwa nawe.Umenipandisha juu

mawinguni.Umeniheshimisha. Hakuna aliyefahamu lakini tayari nilikuwa ninaogelea vumbini lakini wewe ukaniokota na kunipukuta vumbi ukanivisha mavazi na sasa ninaonekana mtu tena” alisema Latoya

“Tafadhali Latoya usiseme hivyo”

“Huo ndio ukweli ambao sioni aibu kuusema.Umenipa kile ambacho kila mwanamke anatamani kukipata yaani nafasi ya pekee katika maisha yako.Aliyekuwa kuwa Rais wa

Marekani Barak Obama kila alipokuwa akitamka jambo ambalo linawahusu yeye na mke wake alianza kwa kusema *“Michelle and I”*.Alimtangliza kwanza mke wake. Sifahamu wanawake wenzangu wanaliongeleaje jambo hilo lakini kwangu mimi hicho ni kitu kikubwa sana ambacho ninakihitaji kutoka kwa mwanaume na nimekipata kwako Mathew.Ahsante sana” alisema Latoya

“Ni mimi ninayepaswa kukushukuru wewe kwa upendo mkubwa kwangu.Mimi

si malaika nina mapungufu yangu lakini kwa dhati ya moyo wako umeyakubali mapungufu yangu na kubwa zaidi umefahamu kuwa maisha yangu yamezungukwa na hatari tupu lakini hilo kwako si tatizo.Umekubali kusimama nami masika na kiangazi.Wewe ni wa kipekee sana Latoya.Ni mwanaume gani ambaye atashindwa kuufungua moyo wake wote kwa mwanamke wa kipekee kama wewe? Aliuliza Mathew

“Mathew kuna jambo nataka kukujulisha leo” alisema Latoya

“Jambo gani Latoya? Mathew aliuliza.Latoya alitabasamu akatazama chini kwa sekunde chahe halafu alisema

“I’m ready” alinyamaza akamtazama Mathew kwa muda halafu akaendelea.

“Niko tayari sasa kusimama na kula kiapo mbele ya madhabahu.Nina uhakika mkubwa moyo wangu ninauweka katika mikono

salama.” Alisema Latoya.Kauli ile ilimfanya Mathew abaki mdomo wazi huku akitabasamu

“Latoya tafadhali niambie kama unamaanisha hicho ulichokisema” alisema Mathew

“Ninamaanisha Mathew.Niko tayari sasa kufunga ndoa nawe na kuwa mke wako halali wa ndoa” alisema Latoya na mara akajikuta akielea juu baada ya mikono yenye nguvu ya Mathew

kumnyanyua.Walikumbatiana kwa nguvu huku wakibusiana

“Ahsante Latoya.Ahsante sana kwa kukubali kufunga nami ndoa.Hiki ni kitu kikubwa sana katika maisha yangu.Nataka mara tu utakaporejea kutoka Dubai tuanze maandalizi haraka sana bila kuchelewa.Alisema Mathew na kwa furaha aliyokuwa nayo akamuinua tena Latoya wakaelekea chumbani.

PATRA HOTEL

Akiendesha gari la kifahari aina ya Rolls Royce lenye rangi nyeupe,Mathew Mulumbi aliingia katika viunga vya hoteli ya kifahari ya Patra.Kwa mwendo wa taratibu alielekea katika maegesho ya magari hotelini hapo.Alishuka garini akahakiki usalama wake halafu akaanza kupiga hatua kuelekea hotelini.Watu walikuwa wengi kiasi hotelini hapo hivyo alitembea kwa tahadhari kubwa.Aliingia ndani ya hoteli akaelekea mapokezi

akawakuta akina dada watatu waliovalia sare nadhifu.Aliwasalimu mwanadada mmoja ambaye hakuwa akimuhudumia mtu.

“Samahani dada” alisema Mathew

“Bila samahani kaka karibu .Nikusaidie nini? Aliuliza yule mwanadada huku akitabasamu

“Ni mara ya kwanza ninafika hapa .Ninahitaji kufika ukumbi wa Twiga.” alisema Mathew.Yule mwanadada alimuelekeza

namna ya kufika katika ukumbi wa Twiga.Mathew alimshukuru,akageuka na kuanza kupiga hatua kuelekea katika lifti.Ukumbi wa Chita ulikuwa na ghorofa ya sita.Ndani ya lifti alikuwa na akina dada kadhaa waliokuwa wamependeza .Lifti ilipofika ghorofa ya sita ilisimama milango ikajifungua.Watu wote waliokuwa ndani ya lifti wakashuka.

“Kumbe wote tulikuwa tunashuka ghorofa ya sita” Mathew alimwambia mwanadada mmoja ambaye

alitabasamu halafu akatoa kicheko kidogo.Mathew aliwaacha akina dada wale akafuata korido kuelekea ukumbi wa Twiga.Nje ya mlango wa kuingilia ndani ya ukumbi wa Twiga aliwakuta akina dada wawili na mwanaume mmoja waliokuwa na kazi ya kupokea na kuwakaribisha wageni.Aliwasalimu halafu akatoa kadi katika mfuko wa koti akawapatia wakamruhusu akapita akaingia ukumbini.Mara tu alipoingia ndani ya ukumbi mwanadada

mmoja mrefu mwambamba aliyevalia gauni refu jeusi akamfuata akamsalimu halafu akamtaka amfuate.Mwanadada yule na wenzake kazi yao ilikuwa ni kuwapanga wageni ndani ya ukumbi.Moja kwa moja alimuongoza Mathew hadi katika meza iliyokuwa na jamaa wawili.Alimuuliza kinywaji anachokitumia halafu akaondoka.Baada ya dakika chache kinywaji alichohitaji Mathew kikaletwa

“Ama kweli sherehe imeandaliwa vilivyo.Watu

wamependeza isivyo kawaida” aliwaza Mathew akiendelea kupitisha macho ukumbini mle.Alichukua simu yake akaandika ujumbe mfupi

“*Gosu Gosu,mimi tayari nimefika ila sikuoni ukumbini”*

Baada ya sekunde chache ukaingia ujumbe

“Karibu sana Mathew.Nimebanwa kidogo ila sherehe itakapoanza tutaonana” alijibu Gosu Gosu.

Mathew Mulumbi na wageni wengine wote waliokuwamo ndani ya ukumbi ule wa Twiga walialikwa katika sherehe ya kumbu kumbu ya kuzaliwa Ambola Lyimo.Ambola ambaye alitimiza umri wa miaka ishirini na nane,ni mmiliki wa kampuni maarufu ya kutengeneza Pizza jijini Dar es salaam.

“Toka nimemfahamu Gosu Gosu hii ni mara ya kwanza kumuona akidumu na mwanamke kwa muda mrefu.Yawezekana ameamua

kuacha kuruka ruka na kutulia na huyu aliyenaye sasa.Ni mwanamke mzuri na kuna kila dalili uhusiano wao utafika mbali sana.Gosu Gosu humuelezi kitu kwa Ambola.Nitaendelea kumsisitiza asirudie tabia zake zile za awali kubadili wanawake kama nguo atulie na huyu aliyempata .Sintomshauri aingie katika ndoa kwanza hadi pale atakapojiridhisha kuwa kweli huyu ndiye mwanamke anayemfaa.” Mathew alitolewa mawazoni na sauti ya

muongozaji shughuli aliyewataka watu wote waliokuwa nje ya ukumbi kuingia ukumbini ili sherehe ianze.

Ilikuwa ni sherehe iliyofana mno.Kila aliyekuwemo ndani ya ukumbi alikuwa na sura iliyojaa furaha.Ulipofika wakati wa zawadi Ambola alijkuta akioga fedha badala ya maji.Kila mwalikwa alijitahidi kujitutumua kumwagia manoti mrembo yule.

“Yawezekana labda mimi ndiye niliyetoa kiasi kidogo zaidi.Nimetoa elfu ishirini wakati wengine wanamwaga mabunda ya noti” aliwaza Mathew akiendelea kushuhudia Ambola akimwagiwa noti

“Siwezi kuonesha ufahari humu ukumbini wakati kuna watu wengi wenye uhitaji wa fedha.Huyu tunayeshindana kumwagia manoti,kwanza anatoka katika familia yenye uwezo mkubwa,vile vile yeye mwenyewe ana biashara kubwa inayomuingizia pesa

nyingi.Kuna watu wengi wanashida kubwa ambao wanahitaji tuwasaidie ndiyo maana nimeanza ujenzi wa kituo cha kulelea wazee na watu wasiojiweza.Mungu amenibariki akanipatia utajiri hivyo natakiwa kutumia sehemu ya utajiri huo pia kwa ajili ya kuwasaidia wengine" aliwaza Mathew akiendelea kushusha mvinyo taratibu

Matukio yote yaliyotakiwa kufanyia yalimalizika na baada ya chakula ulikuwa ni wakati wa kucheza mziki.Aliyeufungua mziki

alikuwa ni Ambola na baba yake jaji mstaafu Bryson Lyimo.Baada ya muziki kufunguliwa ulikuwa ni wasaa wa wageni wote kujumuika ukumbini kusakata dansi.

“Naona mambo yamemalizika hapa.Mimi si mpenzi wa muziki hivyo ni wakati wangu wa kuondoka” aliwaza Mathew akachukua simu akamuandikia ujumbe Gosu Gosu

“Ninaondoka tutaonana kesho.Hongera kwa sherehe imefana sana” Mathew

alimuandikia ujumbe Gosu Gosu halafu akainuka na taratibu akatoka mle ukumbini akaelekea moja kwa moja garini kwake akaondoka.

Baada ya kuondoka ukumbini Mathew alielekea moja kwa moja nyumbani kwake Matanki saba.Geti lilifunguka akaingia ndani,moja kwa moja akaelekea katika nyumba ya kuhifadhi gari nako lango lilijifungua akaingiza gari ndani.Vitu vingi katika jumba la kifahari la Mathew Mulumbi vilikuwa viliendeshwa

kielektroniki.Alipoingia chumbani kwake Mathew aliingia bafuni kuoga kabla ya kulala.Kisha oga alipiga magoti kumshukuru Mungu kwa siku ile halafu akapanda kitandani.

****

Gosu Gosu alihisi mikono laini ikipita katika kifua chake.Alihisi ulimi ukizunguka ndani ya sikio lake taratibu.Alihisi msisimko wa ajabu.Mara alipigwa busu zito mdomoni.

“I love you Ambola” alisema Gosu Gosu kwa sauti iliyojaa uchovu na usingizi.Bado alikuwa ameyafumba macho yake.Mikono ile laini ilishuka taratibu hadi maeneo ya ikulu.Taratibu kulianza kufura. Gosu Gosu alihisi damu ikimchemka.Mikono ile laini iliendelea na utundu wake ikulu huku midomo laini ikiganda katika mdomo wa Gosu Gosu.Akiwa bado amefumba macho Gosu Gosu alihisi ikulu kukizama katika unyevu ishara kuwa mtanange

ulikwisha anza.Miguno ilianza kusikika na mara ghafla mlango ukafunguliwa, sauti kali ikasikika

“What the hell !!

Ilikuwa ni sauti kali ya mwanamama iliyomshtua Gosu Gosu akafumbua macho.Hakuamini macho yake kwa kile alichokiona.Ni kitu ambacho hakuwa amekitarajia kabisa.

“Elizabeth ?!! alisema kwa mshangao.Mwili wote uliingiwa baridi.Ikulu kukapoa ghafla.

Gosu Gosu alikuwa kitandani akiwa mtupu.Juu yake alikuwepo Elizabeth mdogo wake Ambola naye akiwa mtupu.Kitanda kilivurugwa.Mashuka na mito vyote vilikuwa chini.Hali iliyokuwemo mle chumbani ilionesha dhahiri kulifanyika mchuano mkali sana usiku.Mita chache kutoka kitanda alisimama mwanamama mmoja mnene akiwa na sura iliyojaa hasira.Kwa hasira alizokuwa nazo kama angekuwa na silaha angeweza kuua.

Gosu Gosu alimsukuma Elizabeth akashuka chini ili kuokota nguo zake avae,ghafla yule mama alichukua chupa iliyokuwa mezani akairusha Gosu Gosu akaikwepa.Aliinua stuli akairusha Gosu Gosu akaipangua kwa mkono wake wa kulia.Yule mama akamfuata Gosu Gosu na kuanza kumnasa makofi.

“Shetani wa mguu mmoja wewe ! Wanawake wote hawa wamejaa mitaani hujawaona hadi umfuate binti yangu ?! Ni kiumbe wa aina gani wewe mwenye laana unatembea na

dada na mdogo wake?! Aliuliza yule mama kwa ukali akiendelea kumnasa Gosu Gosu makofi.Gosu Gosu akaikamata mikono ya yule mama

“Mama samahani.Sifahamu jambo hili limetokeaje ! alisema Gosu Gosu huku akiendelea kushangaa

“Vaa nguo zako uondoke humu haraka sana mzinzi mkubwa wewe ! alifoka yule mama.Haraka haraka Gosu Gosu aliokota nguo zake

akavaa.Bado yule mama alikuwa anamtazama kwa macho yaliyojaa hasira huku akitweta.Wakati akifunga vifungo vya shati yule mama alisema kwa ukali

“Nipe namba yako ya simu!

Gosu Gosu alimpatia namba yake ya simu

“Ondoka humu haraka sana shetani wewe lakini kwa hiki ulichonifanyia mimi nawe bado hatujamaliza.Nitakutafuta! alisema yule mama kwa

hasira.Gosu Gosu akatupa jicho kitandani hakumuona tena Elizabeth.Nguo zake bado zilikuwa chini .Alihisi amekimbilia chooni.

Gosu Gosu alipotoka nje alipata wazo la kutazama juu ya mlango kusoma namba ya chumba,alizidi kuingiwa na hofu.Chumba kile alichokuwamo kilikuwa namba 309.Chumba ambacho alikodi kwa ajili ya kulala na mpenzi wake Ambola ni chumba namba 312.Alisimama nje ya kile chumba akiutazama mlango ule.Kichwa kilijaa

mawazo.Alihisi miguu inamuisha nguvu.

“Haya ni maajabu makubwa.Sielewi jambo hili limetokeaje.Hii ni aibu ya karne” aliwaza halafu akaanza kupiga hatua kuelekea katika chumba namba 312.Alisimama nje ya mlango wa kile chumba akasita kuufungua mlango.

“Nitamjibu nini Ambola akiniuliza mahala nilikolala usiku? Alijiuliza

“Dah ! leo nimeumbuka.Sikutegemea kabisa.Tukio lile

limetokeaje?”aliendelea kuwaza.

Alitumia dakika tatu pale mlangoni mwishowe aliamua kuingia ndani.Alikinyonga kitasa mlango ukafunguka.Mara tu alipoingia chumbani picha aliyoikuta ilimshtua sana.Ambola alikuwa amelala kitandani akiwa mtupu kabisa.Kitanda alicholala kilionesha ni dhahiri usiku ule kulikuwa na shughuli pevu pale kitandani.

“Hii hali inaonesha wazi kuna shughuli ilifanyika humu

usiku.Mbona sikumbuki chochote? Ni mimi ndiye niliyefanya haya? Nilitokaje humu ndani na kwenda katika chumba kile cha Elizabeth? Alijiuliza Gosu Gosu akiwa amesimama hatua chache kutoka mlangoni.Mara ghafla Ambola akafumbua macho

“Oh darling.Please come over.I feel cold.I need a hug” alisema Ambola akionekana kuchoka sana.Gosu Gosu alivuta pumzi ndefu.Haraka haraka alivua nguo zake akazitupa katika sofa akapanda kitandani.Bado

alihisi woga mkubwa.Mambo yaliyotokea yalimcha nganya.

“Please hug me tight! Alisema Ambola.Gosu Gosu akamkumbatia kwa nguvu.

“Ama kweli hii dunia imejaa maajabu makubwa.Kilichonitokea ni kitu cha ajabu sana” aliwaza Gosu Gosu

****

Saa kubwa yenye rangi ya dhahabu iliyokuwa ukutani ilitoa mlio kuashiria ni saa nne kamili asubuhi.Mlio ule

ulimshtua Ambola akageuka upande wa pili alikolala Gosu Gosu,akamkumbaia halafu akampiga busu zito.

“Darling sina maneno mazuri ya kukushukuru.Toka ndani ya moyo wangu nasema ahsante sana.Ulichonifanyia jana ni kitu kikubwa mno” alisema Ambola.Kwa mara ya kwanza toka asubuhi,Gosu Gosu alitabasamu

“Usijali mpenzi wangu.Niko tayari kufanya chochote katika dunia hii ilimradi uwe na furaha ndani

ya moyo wako.Hata ukiniambia nikakuletee mchanga wa mwezini nitakwenda mpenzi wangu" alisema Gosu Gosu.Ambola akacheka halafu akambusu.

"Nina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kunipa mwanaume kama wewe Gosu Gosu.Wewe ni wa kipekee kabisa.Tafadhali naomba usiugawe moyo wangu kati kati" alisema Ambola

"Ninakupenda sana Ambola.Ninakuahidi katu

sintakutoa chozi.Nitafanya kila linalowezekana kufanyika ili uwe ni mwanamke mwenye furaha kuliko wote duniani” alisema Gosu Gosu.Ambola alimkumbatia kwa nguvu.

“Natamani niendelee kukukumbatia hivi kwa siku nzima ya leo” alisema Ambola

“Hata mimi natamani ingekuwa hivyo lakini bado tuna mambo mengine ya kufanya siku ya leo” alisema Gosu Gosu na kuinuka akakaa.Ambola naye aliinuka akajinyoosha

“Mwili wote umevunjika vunjika.Jana nilikunywa pombe nyingi halafu na wewe uliponikamata hukuniachia.Ulikuwa na nguvu kama Simba ” alisema Ambola huku akicheka.Gosu Gosu naye alitoa kicheko lakini kauli ile ilimuongezea maswali mengi kichwani.Alijitahidi kucheka ili Ambola asiweze kugundua kama ana tatizo linamsumbua

“Kuna wakati nilishtuka usingizini nikakukosa kitandani.Ulikwenda wapi? Aliuliza Ambola.Swali lile lilikuwa ni kama jiwe kubwa

limetua katika kichwa cha Gosu Gosu

“Ni kweli nilitoka kwenda kuhakikisha kila kitu kiko sawa kule ukumbini.Nataka kuwakabidhi hoteli ukumbi wao ukiwa salama”

“Kila kitu kiko salama? Aliuliza Ambola.

“Kila kitu kiko shwari.Hakuna uharibifu wowote uliofanyika”

“Hilo ni jambo la kushukuru sana.Mpenzi nataka kabla hatujaondoka

nikutambulishe kwa familia yangu.Mama aliniambia ana hamu sana ya kukufahamu.” alisema Ambola.Kauli ile ilimshtua sana Gosu Gosu.Ukapita ukimya

“Mbona umeshtuka Gosu Gosu? Aliuliza ambola

“Nadhani tungetafuta siku maalum ya kufahamiana na familia yako lakini si leo.” alisema Gosu Gosu

“Usiwe na hofu mpenzi wangu.Tayari wanakufahamu ila wewe na wao hamjawahi kukutana na kutambuana

rasmi.Ni utambulisho mfupi tu kabla ya ule rasmi” alisema Ambola

“Ambola si kwamba sitaki kuonana na wazazi wako la hasha.Nitaonana nao lakini si siku ya leo.Tupange siku nyingine tutakwenda kuonana nao” alisema Gosu Gosu

“Too late.Tayari nimekwisha wapa taarifa kuwa leo tutakuwa nawe kwa chakula cha mchana hapa hotelini.Sikukupa taarifa mpenzi ila baba,mama na

Elizabeth wote wamelala hapa hapa hotelini”alisema Ambola

“Wamelala hapa? Aliuliza Gosu Gosu akionekana kushangaa

“Ndiyo.Niliwachukulia vyumba hapa hapa hotelini.Sikutaka warejee nyumbani usiku.Baadaye mchana tutakutana kwa ajili ya chakula.Usiwe na wasi wasi wowote mpenzi kila kitu kitakwenda vizuri.Wazazi wangu hawana tatizo kabisa” alisema Ambola.Gosu Gosu

alishindwa kukataa lakini kwa ndani alikuwa anatetemeka.

“Nitawezaje kutazamana usoni na yule mama? Nikiendelea kukataa nitamuumiza Ambola na anaweza akaanza kuhisi kuna tatizo au mimi ni mlaghai ndiyo maana sitaki kuonana na wazazi wake.Huu ni mtihani mkubwa sana.Hata hivyo ngoja nivae miwani ya mbao nijifanye kama vile hakuna chochote kilichotokea.Baada ya leo lazima nimtafute Elizabeth anieleze kile kilichotokea jana kwa sababu

sina kumbu kumbu yoyote nini kilitokea nikajikuta katika chumba chake.Sikuwa nimekunywa pombe nyingi za kunifanya nipoteze kumbu kumbu.Kinachonishangaza zaidi ni kwamba Elizabeth alionekana kufurahia kitendo kile.Hakuwa na wasiwasi hata kidogo.Nini kinaendelea hapa? Alijiuliza halafu akamtazama Ambola kwa jicho la wizi

“Ambola anadai jana nilifanya naye mapenzi karibu usiku mzima.Kama ni kweli imekuaje nikaamkia chumbani kwa Elizabeth? Halafu kitu cha

ajabu nguo zangu zote nilizovaa jana usiu zilikuwa chumbani mle tena inaonekana nilizivua kwa haraka haraka sana.Zilikuwa zimetawanyika sakafuni.Haya ni mauza uza gani yananitokea? Aliendelea kuwaza

“Mpenzi wangu tuamke tukaoge tupate kifungua kinywa. Tunatakiwa tuanze kujiandaa mapema kwa ajili ya chakula cha mchana wa leo na wazazi wangu” alisema Ambola wakainuka wakaelekea bafuni kuoga

****

Kengele ya mlango ililia.Ambola aliinuka akajifunga taulo akaenda kuufungua mlango.Alikuwa ni muhudumu aliyekuwa amerejesha nguo za Gosu Gosu zilizokwenda kufuliwa ambazo alitegemea kuzivaa mchana atakapokutana na familia ya Ambola.

Ilikaribia saa saba mchana muda ambao Ambola na Gosu Gosu walitakiwa kukutana na familia ya Ambola kwa chakula cha mchana. Tangu alipongia

chumbani mle asubuhi akitokea katika chumba cha Elizabeth,Gosu Gosu hakuwa ametoa nje mguu wake.Alikuwa na wasiwasi mwingi.

Baada ya nguo kuletwa walianza kujiandaa kwa ajili ya kutoka.Maandalizi yalipokamilika Gosu Gosu alijitazama katika kioo akavuta pumzi ndefu.

“Sina namna nyingine ya kufanya lazima nikaonane na familia ya Ambola.Kinachonipa hofu ni

mama yake.Je atanikubali baada ya kushuhudia nilichokifanya? Amenikuta nikiwa kitandani na mdogo wake Ambola,sina hakika kama anaweza akakubali kukaa meza moja na mimi.Ni vipi kama akimueleza Ambola kile kilichotokea? Ambola ataumia mno kitu ambacho sitaki kitokee.Ngoja tu niende huko japo naamini lazima moto utawaka.Nilimuona yule mama namna alivyokuwa ananitazama asubuhi.Kama angekuwa na silaha mkononi naamini

angenimaliza.Alinitazama kwa jicho la kikatili” aliwaza Gosu Gosu

“Darling are you okay? Aliuliza Ambola baada ya kumuona Gosu Gosu ametumia muda mrefu katika kioo

“Im okay my love.Lazima nihakikishe muonekano wangu ni nadhifu kabla ya kukutana na familia yako” alisema Gosu Gosu akamvuta Ambola akambusu.

“Uko tayari? Aliuliza Gosu Gosu akijiahidi kutokuonesha wasiwasi wowote

“Mimi niko tayari ninakusubiri wewe” alisema Ambola.Akamkumbatia Gosu Gosu akambusu

“Darling are you sure you want to do this? Aliuliza Ambola

“Yes” alisema Gosu Gosu na kumtazama Ambola

“Nataka kuonana na familia yako.Ni vyema wakafahamu mtoto wao yuko

na nani katika mahusiano” alisema Gosu Gosu.Ambola alichukua simu ya chumbani akapiga hotelini akawataka waanze kuandaa ile meza aliyokuwa ametoa oda.Wahudumu walifanya kazi yao kwa haraka na ndani ya muda mfupi tayari meza likwisha andaliwa,Ambola akajulishwa.Walitoka chumbani wakaelekea bustanini ambako ndiko meza yao ilikoandaliwa.Meza ilichafuliwa kwa vyakula vya aina mbali mbali.Baada ya kuridhika na maandalizi

yale,Ambola aliwapigia simu wazazi wake akawajulisha kuwa kila kitu tayari .Gosu Gosu alivuta pumzi ndefu

“Usihofu darling.Hakuna tatizo lolote.Wazazi wangu ni watu wazuri sana.Naamini wewe mwenyewe utawafurahia” alisema Ambola

“Huyu Ambola ni kama vile anayasoma mawazo yangu kuwa sitaki kuonana na familia yake.Hata hivyo maji nimeshayavulia nguo lazima niyaoge.Nitajikaza kiume kama vile hakijatokea kitu”

aliwaza Gosu Gosu akiendelea kukata mvino taratibu

Dakika tano baadaye walitokea wazazi wa Ambola.Nyuma yao alikuwepo Elizabeth.Alikuwa ameyafunika macho yake kwa miwani mikubwa myeusi.Ambola na Gosu Gosu walisimama wakawasalimu wazee wale wakawakaribisha mezani.Elizabeth aliwasalimu Ambola na Gosu Gosu naye akaketi,hakuonesha wasiwasi wowote.Gosu Gosu alihisi kutetemeka kwa ndani

alipogonganisha macho na mama yake Ambola

Ambola aliongoza maombi kuombea chakula kile halafu wakaanza kujihudumia kila mmoja chakula alichokipenda.

“Nimeipenda hoteli hii.Ina hadhi ya kimataifa.Huduma zao kuanzia chakula na kila kitu ni nzuri sana” alisema baba yake Ambola

“Baba na mama nimeandaa chakula hiki maalum siku ya leo kwanza kuwashukuruni sana kwa malezi yenu hadi kunifikisha

hapa nilipofika ambapo ninaweza kujitegemea mwenyewe japokuwa bado nahitaji malezi yenu kwani mtoto hakui kwa wazazi” alisema Ambola.Alichukua glasi yenye mvinyo mwepesi akanywa funda moja halafu akaendelea

“Pamoja na shukrani hizo za kipekee kwenu,nimeona si vibaya katika chakula hiki nikawajulisha japo siyo rasmi kuwa ninaye mwenzangu ambaye niko naye katika mahusiano.Nimemualika naye kujumuika nasi leo na vile vile

kuifahamu familia yangu” alisema Ambola na kumtazama Gosu Gosu.Macho ya Gosu Gosu yalizunguka haraka haraka kuwatazama wazazi wa Ambola ambao wote walionekana kuwa na nyuso zenye tabasamu.

“Anaitwa Papi Gosu Gosu.Ni mmiliki wa ile kampuni kubwa ya kutengeneza maziwa ya Hello Tanzania.Nimekuwa naye katika mahusiano kwa muda wa mwaka mmoja sasa hivyo si vibaya kumtambulisha kwenu mumfahamu” Ambola alisema

huku akiwatazama wazazi wake.Macho yake yalionesha wasiwasi pia.

“Gosu Gosu hawa ni wazazi wangu.Baba yangu jaji mstaafu Perfect Lyimo.Mama yangu Bernadetha Lyimo na mdogo wangu Elizabeth ambaye yeye tayari unamfahamu.Karibu sana hii ndiyo familia yangu” alisema Ambola.Mzee Lyimo alichukua kipande cha nyama akatafuta halafu akashushia na kinywaji.Alimtazama Gosu Gosu na kusema

“Bwana Gosu Gosu karibu sana katika familia yetu.Tumefurahi kukuona.Kitendo cha kukubali kuja kukutana nasi leo hii kinaonesha ni namna gani ulivyo muungwana na mwenye adabu.Hiki ni kiashiria kuwa una malengo mazuri na mwanetu.Ametuambia mmekuwa katika mahusiano kwa muda wa mwaka mzima.Ni kipindi kirefu ninaamini hadi mmefikia hatua hii ya kuja kukutana nasi tayari kila mmoja amemkubali mwenzake.Mimi kama baba

sina tatizo lolote
nakukaribisha sana ila ninatoa angalizo tu kuwa ,sitaki uuvunje moyo wa huyu binti.Mara nyingi nimekuwa nikimuasa kutafuta mwanaume mwenye malengo naye makubwa.Si mwanaume yule ambaye anavutiwa na uzuri wake.Nataka mwanaume ambaye hata ikitokea mwanangu akapata matatizo au ajali leo akapoteza viungo au uzuri wake bado ataendelea kumuona yu mzuri kama alivyokutana naye mara ya kwanza.Naamini amelizingatia

hilo ndiyo maana leo hii ametukutanisha nawe.Yangu mimi ni hayo machache.Ninawatakia kila la heri katika mahusiano yenu” alisema jaji mstaafu Perfect Lyimo.Gosu Gosu aliweka mikono kifuani akimshukuru mzee yule kwa maneno yake

“Mimi kwa upande wangu sina tatizo lolote.Kama Ambola amemkubali mwenzake sisi hatuwezi kutia neno .Ninaamini mna malengo makubwa maishani mwenu na nitaomba kuanzia sasa mambo yaende haraka haraka.Kama

kila mmoja amemkubali mwenzake kwa nini kuendelea kuvuta muda? Taratibu za ndoa zianze mara moja.Yangu ni hayo tu” alisema mama yake Ambola.Gosu Gosu alishukuru pia.Kijasho kilikuwa kinamtoka usoni.Hakuamini kusikia maneno ya yule mama ambaye asubuhi alimfuma chumbani na Elizabeth mdogo wake Ambola.

“Elizabeth unasemaje? Umemuona shemeji yako? Una mkubali? Aliuliza mama yake Ambola

“Mimi sina tatizo naye.Nimemfahamu muda mrefu kidogo lakini sikuwahi kuwaambia chochote.Ni mtu mzuri.Dada amefanya chaguo sahihi.Karibu sana shemeji Gosu Gosu”alisema Elizabeth.Ilimlazimu Gosu Gosu achukue kitambaa na kujifuta usoni.Alihisi joto.Bomu alilolitegemea kulipuka halikulipuka.

“Ninawashukuru sana wazazi wangu kwa kumpokea mwenzangu. Ninawahakikishia kuwa sikukurupuka kumchagua Gosu Gosu.Ni mtu

mwenye sifa zote za mwanaume yule ninayemuhitaji katika maisha yangu.Ninataka kuwahakikishia vile vile kuwa huu siyo utambulisho rasmi.Gosu Gosu atakuja rasmi kujitambulisha kwetu na ndugu wote wataitwa kutambulishwa kama zilivyo taratibu.Malengo yetu ni kufunga ndoa kama alivyoshauri mama.Hivyo nawatoa wasiwasi kuwa muda si mrefu sana mambo yataanza” alisema Ambola

“Hayo ndiyo maneno niliyotaka kuyasikia” alisema mama yake Ambola halafu wote wakawa kimya wakayaelekeza macho yao kwa Gosu Gosu ishara kuwa walikuwa wanasubiri neno kutoka kwake.Alikohoa kidogo kisha akasema

“Baba,mama na Elizabeth sina mengi ya kusema.Kubwa ninawashukuru sana kwa kunipokea na kunikubali.Ninawahakikishia wazee wangu kuwa mwanenu nitamtunza na kumlinda.Sintamtoa chozi

hata mara moja.Kama alivyosema mwenyewe,tunajiandaa kwa utambulisho rasmi kisha taratibu nyingine zianze.Kwa leo naomba niseme hayo machache.Narudia tena kuwashukuru kwa kunikubali” Gosu Gosu alisema machache

“Bwana Gosu Gosu wewe unatokea mkoa gani hapa Tanzania? Aliuliza mzee Perfect

“Mimi asili yangu ni jamhuri ya kidemokrasia ya Congo lakini kwa sasa tayari ni

raia wa Tanzania” alijibu Gosu Gosu

“Wazazi wako wote wako hai? Aliuliza mama Ambola

“Wazazi wangu wote wamekwisha fariki” alijibu Gosu Gosu

“Pole sana.Ndugu wengine kama wajomba mashangazi wapo? Aliuliza mzee Perfect

“Kujibu swali hilo labda niwape historia yangu kwa ufupi.Mimi nilizaliwa kijijini.Nikiwa na umri wa miaka saba kijiji chetu

kilivamiwa na waasi wakaua watu wengi wakiwamo wazazi wangu.Mimi na watoto wenzagu wapatao mia moja na ishirini tukakamatwa tukapelekwa msituni kupewa mafunzo ya kijeshi.Baadaye tulikombolewa na vikosi vya serikali ya Congo tukapelekwa kutunzwa katika makambi yaliyokuwa yameandaliwa,tukasomeshwa. Baada ya kuwa mkubwa nikaondoka Congo na kuja Tanzania.Siwakumbuki tena ndugu zangu walioko Congo.Ndugu zangu mimi ni

watanzania” alisema Gosu Gosu

“Dah ! pole sana kwa yote uliyopitia” alisema mzee Perfect.Waliendelea kupata chakula huku wakizungumza mambo mbali mbali kuhusiana na biashara.Baada ya kumaliza kupata chakula mze Perfect aliwashukuru Gosu Gosu na Ambola kwa mwaliko ule wa chakula cha mchana akawaaga.Wote walisimama na kuanza kuondoka.

“Mkwe kuna jambo nataka kuzungumza nawe.Ninyi

wengine tangulieni nitawakuta” alisema mama yake Ambola.Wengine wote waliondoka isipokuwa Gosu Gosu.

“Kesho saa tatu asubuhi nataka ufike Samawati beach hotel.Nitakutumia ujumbe kukupa namba ya chumba.Nina mazungumzo nawe.Umenielewa Gosu Gosu? Aliuliza yule mama kwa ukali

“Nimekuelewa mama” alijibu Gosu Gosu

“Good.Ni hilo tu nililotaka kukueleza” alisema mama yake

Ambola wakainuka na kuondoka kuwafuata akina Ambola.

****

Gosu Gosu alirejea nyumbani kwake akaelekea moja kwa moja chumbani akakaa kitandani

“Sasa ni wakati wangu wa kutafakari kile kilichonitokea usiku wa jana.Nimejaribu kutafakari sana kilichotokea sijapata jibu.Naamini nikiwa katika utulivu mkubwa

nitaweza kupata jibu” aliwaza Gosu Gosu akaweka muziki laini wa ala akaanza kutafakari kuhusu usiku wa jana.Alivuta kumbu kumbu kuanzia asubuhi ya siku ya jana hadi walivyoingia ukumbini katika sherehe.Alivuta kumbu kumbu ya matukio yote sherehe lakini hakukumbuka sherehe ilifungwa saa ngapi na aliondokaje ukumbini.

“Je sikuwemo ukumbini hadi mwisho wa sherehe? Alijiuliza

“Kama nilifika hadi mwisho wa sherehe inakuaje ninashindwa kukumbuka namna nilivyotoka ukumbini? Au nililewa sana hadi nikapoteza kumbu kumbu? Aliendelea kujiuliza

“Natakiwa kuwasiliana na Elizabeth.Niliamka nikiwa katika chumba chake hivyo anaweza akafahamu ni namna gani nilifika chumbani kwake.Yawezekana nilikuwa nimelewa nikapoteza kumbu kumbu nikaingia katika chumba chake.Kama ni hivyo kwa nini naye hakutoa taarifa

ili nirejeshwe katika chumba changu?Hapa kuna mambo ambayo nashindwa kuyaelewa” aliwaza Gosu Gosu akachukua simu akaiwasha akaitafuta namba ya simu ya Elizabeth akampigia

“Hallow” ilisema sauti ya Elizabeth

“Elizabeth we need to talk” alisema Gosu Gosu

“Tuzungumze nini? Elizabeth aliuliza

“Kuhusu kile kilichotokea usiku wa jana”

“Forget about last night.Leo ni siku nyingine yaliyotokea jana yamekwisha pita.Ile ni kama ajali ya barabarani hutokea bila mtu kujua”alisema Elizabeth

“Nilifikaje chumbani kwako? Aliuliza Gosu Gosu

“Nimekwisha sema sitaki kulizungumzia suala lile kwani limekwisha pita”

“Tafadhali Elizabeth.Nataka kufahamu kila kitu kilichotokea.Nilifikaje chumbani kwako? Kwa nini ukakubali kulala nami wakati

ukijua mimi niko katika mahusiano na dada yako? Aliuliza Gosu Gosu

“Tell me one thing Gosu Gosu.Did you enjoy the night? Aliuliza Elizabeth.Gosu Gosu alibaki kimya.

“Ukimya huo ni ishara kuwa uliufurahia usiku wa jana pamoja nami.Nilifurahi pia.Nategemea siku zijazo tukawa na usiku kama wa jana.Nakupenda” alisema Elizabeth na kukata simu.Gosu Gosu alibaki na mshangao mkubwa

“Is this real? Alijiuliza

“Huyu Eliza mbona ananishangaza .Badala ya kuona haya yeye anafurahia kulala na mpenzi wa dada yake. Swali ambalo nalitafutia majibu bado ni namna gani niliweza kuondoka ukumbini na kujikuta chumbani kwa Elizabeth? Nataka nitafute majibu kabla Ambola hajalifahamu jambo hili” aliwaza Gosu Gosu

“Nahisi kama kichwa kinataka kunipasuka kwa mawazo.Ngoja nikazungumze

na Mathew Mulumbi.Pengine anaweza akanipa msaada wa mawazo nini nifanye kulitatua jambo hili” Gosu Gosu alichukua simu akampigia Mathew

“Hatimaye umepatikana.Ulikuwa umejificha wapi Gosu Gosu? Mathew aliuliza

“Mathew uko wapi? Nahitaji kukuona”

“Kwema huko lakini? Mathew aliuliza

“Kwema kaka.Uko nyumbani?

“Ndiyo niko nyumbani kwangu”

“Ninakuja hapo sasa hivi” alisema Gosu Gosu.Hakupoteza muda akaingia garini akaondoka kuelekea kwa Mathew Mulumbi

****

“Hongera sana kwa sherehe ya jana.Ilifana mno” alisema Mathew baada ya

Gosu Gosu kufika nyumbani kwake

“Ahsante.Ninakushukuru pia kwa kufika” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu are you okay? Mathew alimuuliza Gosu Gosu baada ya kugundua kuna jambo linamsumbua

“Mathew I need something strong to drink” alisema Gosu Gosu akainuka na kuelekea mahali ambako Mathew huhifadhi chupa za mvinyo akachagua mvinyo

akarejea sebuleni akamimina katika glasi akakata wote.

“Mathew nina mambo mazito yananikabili ndugu yako” alisema Gosu Gosu

“Nieleze tafadhali jambo gani? Umeua mtu? Mathew aliuliza

“Ni zaidi ya kuua mtu.Nimekalia bomu” alisema Gosu Gosu

“Nakusikiliza Gosu Gosu .Nieleze kila kitu”

Gosu Gosu alivuta pumzi ndefu halafu akasema

“Jana kuna tatizo kubwa limenitokea” alinyamaza kidogo

“Mimi na Ambola tulichukua chumba pale pale hotelini ili tupumzike baada ya sherehe.Kitu cha ajabu asubuhi ya leo nimejikuta nikiwa mtupu katika chumba cha Elizabeth mdogo wake Ambola.Kibaya zaidi aliyetufuma ni mama yake Ambola” alisema Gosu Gosu.Mathew alimtazama kwa sekunde kadhaa halafu akasema

“Gosu Gosu naomba tulia nieleze taratibu kila kitu kilichotokea” alisema Mathew.Gosu Gosu alimueleza kilichotokea.

“Dah ! kweli hili ni bomu.Lakini ulifikaje chumbani kwa Elizabeth? Tuanzie hapo”Aliuliza Mathew

“Hilo ndilo swali ambalo nimejiuliza kwa siku nzima ya leo nimekosa jibu.Sifahamu nilifikaje chumbani humo .Kitu kingine cha ajabu ambacho kinanishangaza ni kwamba Elizabeth

hakuonekana kushtushwa na tukio lile.Alionekana kufurahia.Muda mfupi kabla sijakupigia simu,nilizungumza naye anieleze namna nilivyofika chumbani kwake lakini hakunieleza chochote badala yake aliniuliza kama nilifurahia usiku wa jana.Alienda mbali zaidi akadai kuwa naye pia alifurahi na anategemea tutakuwa na usiku mwingine kama wa jana.Mathew nimechanganyikiwa sijui nifanye nini" alisema Gosu Gosu

“Kingine ni kauli ya Ambola kuwa sikumuachia usiku kucha.Ni kweli leo ameamka akiwa amechoka sana.Mwenyewe anadai ni kazi niliyoifanya usiku wa jana.Najiuliza nilifanya saa ngapi halafu nikaenda chumbani kwa Elizabeth? Aliuliza Gosu Gosu

“Ndugu yangu kweli umekutana na janga hata hivyo unatakiwa utulize akili na kulielewa jambo hili namna lilivyotokea.Swali la kujiuliza ni je ulikuwa umelewa sana kiasi cha kupoteza kumbu

kumbu? Ulitoka na Ambola ukumbini? Aliuliza

“Mathew sikumbuki chochote kama niliondoka na Ambola.Kuhusu kulewa sina kumbu kumbu kama nililewa hadi kupoteza kumbu kumbu.Haijawahi kunitokea nikalewa hadi kumbu kumbu zikanipotea”

“Kama hukulewa nini basi kilitokea? Aliuliza Mathew akimtazama Gosu Gosu kwa macho makali

“I don’t know brother” alijibu Gosu Gosu

“Ulikuwemo ukumbini wakati Ambola alipofungua muziki na baba yake? Mathew aliuliza

“Ndiyo nilikuwepo nikacheza naye kidogo wakatokea marafiki zake wakaanza kucheza naye mimi nikaenda kukaa ”alijibu Gosu Gosu

“Unakumbuka nini kiliendelea baada ya hapo? Aliuliza Mathew.Gosu Gosu alizama mawazoni

“Umeme ulipokatika ulikuwemo ukumbini? Aliuliza Mathew

“Umeme ulikatika? Gosu Gosu alishangaa

“Ndiyo. Wakati muziki ukiendelea umeme ulikatika kwa muda mfupi halafu ukarejea tena” alisema Mathew

“Sina kumbu kumbu kama umeme ulikatika” alijibu Gosu Gosu

“Yawezekana wakati umeme unakatika hukuwemo

ukumbini.Ili tuweze kupata picha halisi ya kile kilichotokea,nataka ufikiri kwa kila kila kitu kuanzia pale ulipoacha kucheza na Ambola ukaenda kukaa kitini.Naamini tatizo lilianzia hapo” alisema Mathew.Gosu Gosu akainamisha kichwa akafikiri kwa muda

“Sikumbuki chochote Mathew.Ni kama vile baada tu ya kukaa ubongo wangu ukaacha kuhifadhi kumbu kumbu ya matukio yaliyoendelea.Sikumbuki tena chochote zaidi ya leo asubuhi

kujikuta chumbani kwa Eliza” alisema Gosu Gosu

“Mh ! hili kweli suala gumu” aliwaza Mathew akimtazama Gosu Gosu

“Gosu Gosu nataka uniambie ukweli bila kunificha.Umekuwa ukiwasiliana na Elizabeth? Aliuliza Mathew

“Elizabeth ni kweli nimekuwa nikiwasiliana naye lakini mawasiliano ya kawaida ya mtu na shemeji yake” alijibu Gosu Gosu

“Hamkuwahi kuzungumza masuala yoyote ya kimapenzi? Hukuwahi kumtamani? Ninakufahamu Gosu Gosu kwa wanawake unaweza ukala kuku na vifaranga wake” alisema Mathew

“Mathew nakiri mimi ninapenda wanawake lakini si kufikia hatua hiyo ya kutembea na mtu na mdogo wake.Ambola ninampenda sana.Hata wewe pia ni shaidi tangu nimekuwa naye tabia yangu ya kubadili wanawake naweza kusema

nimeiacha.Nimeamua kuwa na mwanamke mmoja tu”

“Elizabeth amewahi kuonesha dalili zozote za kukutamani? Mathew aliuliza

“Hajawahi.Ila leo nilipompigia simu alinitamkia kuwa ananipenda”

“Alikutamkia hivyo? Mathew aliuliza

“Ndiyo”

“Picha imeanza kujijenga.Inawezeana Elizabeth amekuwa akikutamani kwa muda mrefu

na akaamua kuitumia nafasi ya jana kutimiza kile ambacho anakitamani.Yawezekana labda ni yeye aliyetengeneza mpango hadi ukajikuta chumbani kwake”

“Kama ni yeye aliwezaje kunirubuni akili? Swali lingine kama aliweza kutengeneza mpango nikalala chumbani kwake nani aliyelala na Ambola kwa usiku mzima? Aliuliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu suala hili linaumiza kichwa.Linahitaji utulivu mkubwa

sana.Nakushauri ujipe muda wa kutafakari kwa kina kila kilichotokea.Nina uhakika mkubwa lazima kuna kitu utakikumbuka kinachoweza kusaidia kujua namna ulivyofika chumbani kwa Elizabeth.Swali lingine mama yake Elizabeth alifahamuje kama umelala chumbani na mwanaye? Mathew aliuliza

“Mathew hili suala zima ninaona kama kiini macho.Sielewi ni uchawi umetumika ama nini” alijibu GosuGosu

“Hakuna kuingiza uchawi hapa Gosu Gosu.Lazima tutafute ni namna gani ulivyoweza kupoteza kumbu kumbu hadi ukajikuta chumbani kwa Elizabeth.Unakumbuka kinywaji ulichokuwa unakunywa? Mathew aliuliza.Gosu Gosu akashtuka akakumbuka kitu

“Mathew naona kama kumbu kumbu zinaanza kurejea.Nimekumbuka wakati Ambola akifungua mziki na baba yake,alinifuata muongoza shughuli akaniambia kuwa

baada ya wazazi wa Ambola kucheza naye mziki,nitakayefuata ni mimi hivyo nijiandae.Baada ya baba na mama yake Ambola kumaliza kucheza watu waliruhusiwa kujimwaga ukumbini nami nikainuka nikaenda kucheza na Ambola”

“Ulipoondoka ulimaliza kinywaji chote katika glasi? Mathew aliuliza

“Niliacha mvinyo nusu nikainuka na kwenda kucheza.Baadae nilirejea kukaa”

“Uliendelea kunywa kinywaji ulichokiacha katika glasi? Mathew aliuliza

“Ndiyo.Niliendelea kunywa kinywaji nilichokiacha katika glasi”Alijibu Gosu Gosu. Mathew alivuta pumzi ndefu

“Hilo ni kosa la kwanza ulilolifanya.Gosu Gosu nimeshiriki nawe katika misheni mbali mbali.Maadui zangu ni maadui zako vilevile.Mahali kokote uliko usimuamini mtu yeyote hata mpenzi wako” alisema Mathew

akiendelea kumkazia macho Gosu Gosu

“Kuna uwezekano uliwekewa kitu katika kinywaji ukapoteza kumbu kumbu na kupelekwa katika chumba cha Elizabeth.Sina hakika,hizo ni hisia zangu tu” alisema Mathew

“Hilo linawezekana Mathew. Hata hivyo kama nilifanyiwa hivyo nini malengo ya hao watu walionifanyia mchezo huo? Nani aliyelala na Ambola usiku mzima? Gosu Gosu aliuliza

“Bado hatuna uhakika kama kuna mchezo ulifanyika wa kukupoteza fahamu.Hizo ni hisia zetu japo inawezekana ikawa hivyo.Kuhusu nani aliyelala na Ambola kwa usiku mzima bado ni swali gumu.Hukulala naye chumbani lakini akakiri umelala naye na kufanya mapenzi usiku kucha.Utanisamehe kwa maneno haya Gosu Gosu lakini lazima tuseme ukweli.Kama si wewe basi kuna mtu aliyelala na Ambola hadi asubuhi”

“Aaaagghhh !! Gosu Gosu aliunguruma kwa hasira

“Mathew kama ni kweli ninaapa nitagonga mlango kwa mlango hadi nimpate mtu huyo.Nitamchuna ngozi yake ! alisema kwa hasira Gosu Gosu

“Gosu Gosu suala hili mtu anaweza akalitazama kama suala la kawaida linaloweza kumtokea mtu yeyote .Mtu anaweza akadhani labda ulilewa sana hadi ukasahau chumba ukajikuta katika chumba cha shemeji yako.Nakubali mambo haya

yapo lakini mimi suala hili nalitazama katika jicho lingine ambalo linanionesha kuna ujinai ndani yake” alisema Mathew

“Mathew unanipa hofu”

“Sikupi hofu Gosu Gosu nakueleza ukweli mtupu kwa namna ninavyoliona hili suala” alisema Mathew

“Nini ushauri wako? Gosu Gosu aliuliza

“Nashauri tuanzishe uchunguzi wa kina na wa kimya kimya wa suala hili ili

tuufahamu ukweli.Kama nilivyokwambia silioni kama ni suala la kawaida hili.Lazima kuna jambo limetokea.Ninakufahamu vyema Gosu Gosu hujawahi kulewa hadi ukapoteza kumbu kumbu.Kuna kitu nyuma ya tukio hilo la jana.Ninachokushauri kwa sasa usimweleze chochote Ambola wala usitake kumuuliza chochote Elizabeth.Tutafanya uchunguzi kimya kimya kujua kile kilichotokea”

“Naamini kabisa mtu aliyenifanyia jambo kama hili lazima atakuwa na malengo ya kuniharibia mahusiano yangu na Ambola.Nina wasiwasi Ambola anaweza akajulishwa juu ya tukio hili kabla hatujakamilisha uchunguzi wetu”alisema Gosu Gosu

“Sina hakika kama malengo ya hao watu ni hayo.Kama malengo yangekuwa ni hayo hivi sasa tayari mngekuwa mmesambaratika tayari.Tutaufahamu ukweli

baada ya kufanya uchunguzi” alisema Mathew

“Mathew ninakwenda kuanza uchunguzi wangu siku ya leo.Nitaanza na yule muongoza shughuli” alisema Gosu Gosu

“Hapana Gosu Gosu hupaswi kufanya hivyo utaharibu mambo.Najua unataka kuupata ukweli kwa haraka lakini hatupaswi kwenda haraka namna hiyo.” alisema Mathew

Waliendelea na mazungumzo hadi ilipotimu

saa nne usiku ambapo Gosu Gosu aliondoka kurejea nyumbani kwake.Akiwa kitandani kwake akiendelea kutafakari ukaingia ujumbe katika simu yake,akaufungua

“Chumba 104”

“Huyu lazima ni mama yake Ambola.Anataka kuniambia nini yule mama? Kwa nini akachagua tukutane hotelini? Yawezekana labda kwa kitendo cha jana hataki niwe na mwanaye.Yawezekana labda anakwenda kuniambia niachane na Ambola.Hakuna

mzazi ambaye anaweza akavumilia kitendo kama kile.Najua wakati ule wa chakula alijitahidi kuficha watu wengine wasifahamu kama kama kuna kitu kinaendelea lakini ndani ya moyo wake ana donge kubwa.Nakumbuka namna alivyonitazama asubuhi ile.Yale ni macho ya kisasi.Kama akinitaka nimuache mwanae sintakuwa na namna nyingine zaidi ya kumueleza ukweli Ambola.Yeye ndiye

atakayeamua hatima yetu” aliwaza Gosu Gosu

****

Ilitimu saa mbili kamili za asubuhi bado Gosu Gosu alikuwa kitandani akitafakari.Bado picha akiwa kitandani na Elizabeth iliendelea kuganda katika akili yake.Taratibu aliinuka pale kitandani akachukua simu akampigia Ambola kumjulia hali

“Hello darling” alisema Ambola

“Uko salama malaika wangu? Aliuliza Gosu Gosu

“Niko salama kabisa.Vipi wewe unaendeleaje? Tayari umefika ofisini? Aliuliza Ambola

“Hapana bado niko kitandani.Nitaelekea huko baadae kidogo asubuhi hii nina miadi ya kukutana na mtu Fulani” alisema Gosu Gosu

“Darling are you okay? Si kawaida yako mida kama hii

kuwa kitandani” alisema Ambola

“Niko kawaida mpenzi usihofu”

“Sawa.Nitaandaa chakula cha jioni leo nyumbani kwangu.Tafadhali usikose” alisema Ambola

“Darlin……” Gosu Gosu alitaka kusema kitu Ambola akamkatisha

“Sihitaji sababu yoyote.Nakutegemea jioni.Uwe na siku njema” alisema Ambola na kukata simu

“Sikutaka kabisa kuonana na Ambola hivi karibuni.Tukio lile limenifanya nianze hadi kumkwepa mpenzi wangu” aliwaza Gosu Gosu akainuka akaenda bafuni kuoga akajiandaa kwa ajili ya kuelekea Samawati beach hotel kama alivyoelekezwa na mama yake Ambola.

Saa nne kasoro dakika kumi na nane Gosu Gosu akiendesha gari aina ya range rover yenye rangi nyeusi aliwasili Samawati beach hotel.Aliegesha gari katika maegesho akashuka na kupiga

hatua haraka haraka kuelekea ndani ya hoteli.Alikitafuta chumba alichoelekezwa akakipata.Alisimama nje ya chumba kile kwa dakika mbili akiwaza huku akiitazama saa yake ya mkononi.Ilipotimu saa nne kamili aligonga mlango.Baada ya sekunde kadhaa mlango ulifunguliwa .Gosu Gosu alihisi kama vile amemwagiwa barafu baada ya kugonganisha macho na mama yake Ambola

“Come in” alisema yule mama.Gosu Gosu aliingia ndani mlango

ukafungwa.Mezani kulikuwa na chupa tatu za mvinyo na sinia lililokuwa na minofu ya kuku.Ilionesha yule mama alikuwa anakunywa mvinyo,hata macho yake yalionesha kuwa alikuwa amekunywa mvinyo mkali.Gosu Gosu akiwa amesimama katikati ya chumba mara alishikwa mkono akasukumwa akaangukia kitandani.Alitaka kuinuka yule mama akamsukuma tena.

“Umezoea kuchezea watoto wa watu.Leo nataka

ucheze na mimi mtu mzima.! Alisema yule mama

“Mama samahani sina mal……” Alisema Gosu Gosu lakini alizuiwa kusema chochote

“Shut up.You are going to do what I say !. Ukitaka uendelee kuwa salama tafadhali fanya kile nitakachokuelekeza” alisema yule mama akimtazama Gosu Gosu kwa macho makali mekundu

“Take off your clothes” alisema yule mama

“No I can’t ! alisema Gosu Gosu akianza kukasirika

“Huyu mama hajanifahamu vizuri mimi ni nani.Asitake kucheza na moto! Aliwaza Gosu Gosu wakati mama Bernadetha akiwa amegeuka akichukua kitu katika pochi yake kubwa.Alichukua bahasha kubwa ya khaki akamrushia Gosu Gosu

“Open it ! alisema Bernadetha.Taratibu Gosu Gosu aliifungua bahasha ile ndani yake akakuta kuna

bahasha nyeupe akaitoa akaifungua.Ndani ya ile bahasha nyeupe kulikuwa na picha zikiwaonesha Gosu Gosu na Elizabeth wakiwa watupu kitandani.Mikono ya Gosu Gosu ilimtetemeka.

“Sitaki useme chochote.Vua nguo zako haraka sana” alisema Bernadetha.Gosu Gosu alifanya kama alivyoelekezwa akabakiwa na nguo ya ndani

“Hiyo pia” alisema Bernadetha.Gosu Gosu aliivua ile nguo ya ndani akabaki

mtupu.Bernadetha akamsogelea akamshika ikulu

“Nataka unioneshe leo ni kitu gani ambacho watoto wangu wote wawili wamechanganyikiwa kwako.Show me ! alisema Bernadetha

“Mama nini unakitaka kwangu? Gosu Gosu aliuliza

“Umetembea na binti yangu wa kwanza ukaona haitoshi ukatembea na wa pili sasa nataka utembee na mimi pia uwe umetumaliza wote !

alisema Bernadetha akianza kuvua nguo.

“Mama tafadhali ! alisema Gosu Gosu

“Nimekwambia sitaki unieleze chochote.Ama unataka picha hizo nimpelekee Ambola? Nakuhakikishai akiziona picha hizo hutamuona tena katika maisha yako”

“Mama kwa nini unanifanyia hivi? Aliuliza Gosu Gosu

“Tafadhali fanya kile ninachokuelekeza halafu tutazungumza” alisema Bernadetha akiendelea kumfanyia Gosu Gosu utundu mwingi.Gosu Gosu aliyekuwa na hasira kama nyati aliamua kukubaliana na kile alichokisema Bernadetha.

Haukuwa mtanange uliochukua muda mrefu sana ukamalizika.Gosu Gosu alikaa pembeni ya kitanda akiwa amejiinamia akijutia kile alichokifanya.

“Thank you” alisema Bernadetha.Gosu Gosu hakumjibu kitu

“It was rough but I enjoyed it” alisema tena Bernadetha huku akiinuka na kuelekea bafuni

“Njoo tuoge tafadhali” alisema Bernadetha

“Mama tafadhali naomba uniambie kile ulichoniitia hapa” alisema Gosu Gosu

“Kuanzia sasa usiniite mama.Niite

Bernadetha.Umesikia? alisema Bernadetha kwa ukali

“Njoo bafuni mara moja.Mambo haya umeyataka mwenyewe usijaribu kuyakwepa” alisema Bernadetha

“Mama sikufanya vile kwa kukusudia.Nilijikuta tu niko chumbani kwa Elizabeth”

“Please stop.Ninao ushahidi wote ambao umekuwa ukimtongoza Elizabeth”

“Mimi?! Gosu Gosu alishangaa

“Tafadhali kijana njoo bafuni haraka” alisema Bernadetha.Gosu Gosu aliingia bafuni wakaanza kuoga.Wakiwa bafuni Bernadetha hakutaka kutoka hivi hivi alihakikisha ametumia kila mbinu hadi ukapigwa mtanange mwingine humo bafuni.

Kisha oga walirejea chumbani kila mmoja akavaa mavazi yake.Bernadetha

alimimina mvinyo katika glasi akampatia Gosu Gosu

“Naamini sasa nafsi yako imeridhika baada ya kutembea nasi wote.Tuachane na hayo.Huo ulikuwa ni utangulizi tu wa kile nilichokuitia hapa” alisema Berbadetha akazichukukua zile picha akazirejesha mkobani.Alitoa diski mweko akaichomeka katika kompyuta yake na kumtaka Gosu Gosu asogee.Kutoka katika ile diski alicheza video iliyomuonesha Gosu Gosu akiwa kitandani na

Elizabeth wakifanya mapenzi.

“Hii ni video ya kweli au imetengenezwa? Alijiuliza Gosu Gosu.Mwili ulimtetemeka

“Sikumbuki kama usiku ule yalitokea mambo kama haya.Mbona ninaonekana nikiwa mzima kabisa na tena nikifurahia kile kinachoendelea? Aliendelea kujiuliza Gosu Gosu.Video ile ilizidi kumchanganya

“Gosu Gosu mpenzi nataka unihakikishie kuwa

utamuacha dada Ambola na kunioa mimi pale nitakapomaliza masomo” alisema Elizabeth akiwa kifuani kwa Gosu Gosu.Wote wawili wakiwa watupu

*“Nakuahidi nitamuacha Ambola.Hakufikii hata robo kwa uzuri wako”*alisema Gosu Gosu

“No ! No ! This is not true.Sijasema maneno haya mimi.Hii ni video ya uongo imetengenezwa kwa lengo la kunichonganisha na Ambola.This is not true”

alisema Gosu Gosu.Kwa hasira aliichukua kompyuta ya Bernadetha akaipiga ukutani.Alisimama kwa hasira akamtazama Bernadetha

“Kwa nini unafanya hivi wewe mama? Aliuliza kwa ukali

“Sit down ! alifoka Bernadetha

“Ninakwenda kumueleza Ambola kila kitu”alisema Gosu Gosu

“Nakuruhusu ukafanye hivyo lakini kabla hujaenda

kwa Ambola kuna jambo ambalo nataka ulifahamu.Kwanza Ambola hatakuelewa na huo utakuwa ni mwisho wenu.Haitaishia hapo.Elizabeth ni mwanafunzi wa kidato cha tano.Unafahamu adhabu ya kufanya mapenzi na kumpa mimba mwanafunzi? Aliuliza Bernadetha.Gosu Gosu alishtuka

“What? Aliuliza Gosu Gosu

“Adhabu kwa kosa hilo la kumpa mimba mwanafunzi ni miaka thelathini gerezani na kazi ngumu.Ninao ushahidi

ukifanya mapenzi na mwanafunzi na sasa mwanafunzi huyo ana mimba.Mume wangu ni jaji mstaafu atatumia nguvu yake aliyonayo kuhakikisha unaozea gerezani.Kijana unakwenda kupotea.Unataka kumalizia maisha yako yote gerezani? Aliuliza Bernadetha akimtazama Gosu Gosu

Kwa kasi ya ajabu Gosu Gosu alimvamia Bernadetha akamsukuma ukutani akamkaba shingo.Ghafla mlango ulifunguliwa wakaingia watu watano wawili

wakiwa na bastola,walimtaka amuache Bernadetha haraka.Gosu Gosu alimuachia Bernadetha akaanguka chini huku akikohoa mfululizo.Mmoja wa wale jamaa walioingia mle ndani alirusha teke Gosu Gosu akaliona akaudaka ule mguu halafu kwa kutumia mkono wake wa kulia wenye nguvu alimvuta yule jamaa akamtandika kichwa kizito akaenda chini.Kwa kasi ya ajabu aligeuka akainua kiti cha mbao kilichokuwa nyuma yake akampiga nacho jamaa

mwingine.Bernadetha aliinuka na kumtaka Gosu Gosu apunguze hasira

“Tafadhlai Gosu Gosu hatuhitaji vurugu”

Gosu Gosu aliwatazma wale jamaa wawili waliokuwa wanagaa gaa chini kwa maumivu

“Hilo ni onyo nmewapa ili mjue mko na mtu wa aina gani.” alisema Gosu Gosu

“Thank you gentlemen.Mnaweza mkaenda” Bernadetha

aliwaambia wale jamaa.Sura ya Gosu Gosu ilizidi kujikunja kwa hasira

“Suala hilo la kudai nimempa mimba mwanafunzi litakufikisha pabaya sana! Alifoka Gosu Gosu

“Sit down ! alifoka Bernadetha

“Unasema nimempa mimba mwanafunzi yupi? Aliuliza Gosu Gosu

“Kila kitu kipo.Ushahidi wa daktari aliyempima mwanafunzi na kumkuta ana

ujauzito upo.Picha zako ukiwa faragha na mwanafunzi huyo zipo na hata video.Huwezi ukakwepa kifungo gerezani.Unachagua nini? Kifungo au kutekeleza kile nikitakacho?Una dakika tatu tu za kufanya maamuzi.” Alisema Bernadetha.GosucGosu alikuwa njia panda hakujua ajibu nini.Bernadetha alisogea dirishani akalifunua pazia halafu akamtaka Gosu Gosu kusogea karibu zaidi.

“Unaona kule maegesho? Kuna gari la polisi ambao

wako hapa kwa lengo moja tu kuhakikisha wanaondoka nawe endapo mimi nawe tutashindwa kuelewana humu ndani" alisema Bernadetha akarudisha pazia.

"You have two minutes to choose" alisema Bernadetha huku akiendelea kumkazia macho Gosu Gosu

"Naamini hauko tayari kwenda gerezani.*Now sit down.We need to talk"* alisema Bernadetha.Gosu Gosu akaketi.

“Nini unakitaka kwangu? Aliuliza Gosu Gosu.Bernadetha alimimina kinywaji katika glasi akanywa.

“Papi Gosu Gosu jana katika chakula ulitueleza historia yako kwa ufupi.Ulitueleza kuwa ulitekwa na waasi ukapelekwa msituni kitu ambacho ni kweli.Ulitudanganya uliposema kuwa mlikombolewa na majeshi ya serikali mkapelekwa katika makambi.Wewe umekuwa muasi hadi miaka michache iliyopita ambapo mlifurushwa

na majeshi ya serikali ukakimbilia Tanzania.Umewahi kumweleza hivyo Ambola? Umewahi kumwambia idadi ya watu uliowaua? Aliuliza Bernadetha.Gosu Gosu hakumjibu kitu

“Hujathubutu kumweleza kwa kuwa unahofu akifahamu historia yako hatakutaka tena. Ninakufahamu Gosu Gosu *you are a killer and a monster !* alisema Bernadetha.Gosu Gosu alizidi kushangaa namna mama yule alivyomfahamu

“Uliniuliza ninataka nini kwako.Kuna kazi ambayo nataka uifanye.Ukiikamilisha hiyo kazi utaishi kwa amani kubwa na mwanangu na hakuna atakayefahamu chochote kuhusu wewe.Kama ukikataa, utaondoka na wale polisi. Utashtakiwa kwa kosa la kufanya mapenzi na mwanafunzi wa shule ya sekondari na kumpa ujauzito.Ushahidi upo wa kutosha tena ni halisi siyo wa kutengeneza.Kesi haitachukua muda mrefu hukumu itatoka utamalizia maisha yako

gerezani.Chaguo ni lako”alisema Bernadetha

“Kazi ipi unataka niifanye? Aliuliza Gosu Gosu.Bernadetha alifungua mkoba wake akachukua bahasha akatoa picha akampa Gosu Gosu

“Unakwenda kumuua huyo mtu pichani”

“Ni nani huyu mtu na kwa nini auawe? Gosu Gosu alihoji

“Hupaswi kuhoji wewe kazi yako ni moja tu kutekeleza maagizo unayopewa.Huyu mtu yuko Arusha na utaondoka

sasa hivi kuelekea huko.Usiku wa leo utamuua halafu utasubiri kuna mtu mwingine ambaye naye utamuua kabla ya kurejea Dar es salaam.Baada ya kazi hizo mbili mimi nawe tutakuwa tumemalizana.” Alisema Bernadetha akimtazama Gosu Gosu

“Naomba unipatie simu yako, utarejeshewa baada ya kuikamilisha kazi yangu.” Alisema tena Bernadetha huku akinyoosha mkono kumtaka Gosu Gosu ampatie simu yake.Gosu Gosu hakukubali

“Gosu Gosu hakuna haja ya kupoteza muda.Nipe simu yako kwa sababu unaondoka sasa hivi kuelekea Arusha” alisisitiza Bernadetha.Gosu Gosu alimkata jicho Bernadetha ambaye alionesha woga kwa mbali

“Nisikilize vizuri.Umeingia mahali pabaya sana hivyo nakushauri uwe makini.Mimi si mtu wa kufanyia mchezo hata kidogo ni mtu mbaya mno na yawezekana bado hujanifahamu vyema.Ninakwenda kuifanya kazi yako kama unavyotaka

lakini nitakapoikamilisha kila kitu kiwe kimekwisha kama tulivyokubaliana.Sitaki tena kusikia chochote kutoka kwako na kama ukikiuka makubaliano haya nakuhakikishia nitakuua wewe na familia yako.Liweke hilo kichwani" alisema Gosu Gosu akaitoa simu yake akaizima halafu akamkabidhi Bernadetha

"Kila kitu utakikuta Arusha.Maelekezo yote kuhusiana na kazi unayokwenda kuifanya utayakuta huko huko

Arusha.Utapelekwa uwanja wa ndege utaondoka na ndege inayoondoka baada ya dakika ishirini kutoka sasa.Hakikisha unaifanya kazi kwa ufundi mkubwa sana” Alisema Bernadetha.

Kimya kifupi kilipita Bernadetha akisubiri kusikia chochote kutoka kwa Gosu Gosu lakini hakusema chochote ishara kuwa alikuwa tayari kwa kazi ile aliyopewa kuifanya.Bernadetha alichukua simu yake akapiga na baada ya muda mfupi wakaingia watu wawili,akamtaka Gosu Gosu

kuongozana na watu wale wakatoka na kuingia garini kwa ajili ya kuelekea uwanja wa ndege tayari kwa safari ya Arusha.

ARUSHA

“Kaka Arusha”alisema jamaa mmoja mwembamba mrefu ambaye macho yake aliyafunika kwa miwani myeusi.Alipuliza moshi wa sigara halafu akamtazama Gosu Gosu

“Ninaitwa Jombaa.Niko hapa kuhakikisha kazi uliyoletwa kuifanya inakamilika kwa ufanisi.” Alisema yule jamaa na kuvuta sigara yake halafu akainuika akaenda katika kabati akatoa bahasha akarejea sofani akaketi.Aliifungua ile bahasha akatoa picha mbili akampatia Gosu Gosu.

“Huyu ndiye mtu uliyekuja kumuondoa hapa Arusha” alisema Jombaa.Gosu Gosu alizitupa picha zile mezani akamtazama Jombaa kwa macho makali

“Ni nani huyu mtu na amefanya nini hadi auawe? Aliuliza Gosu Gosu

“Ndugu utanisamehe kwani hata mimi sina jibu la swali lako.” Alijibu Jombaa

“Kwani ninyi ni akina nani? Aliuliza Gosu Gosu

“Kaka ninachokushauri fanya kile ulicholetwa kukifanya hapa Arusha uondok e zako usitake kujua zaidi.” Alisema Jombaa akavuta tena sigara akatoa moshi mdomoni na puani

“Yuko wapi huyu mtu kwa sasa? Nimeambiwa kila kitu nitaelezwa hapa Arusha”

“Huyu si mwenyeji wa Arusha.Amefikia Kongwa hotel chumba namba 74.Anatumia gari aina ya Prado rangi nyeusi.”Alisema Jombaa

“Inaonekana mmekuwa mkimfuatilia kwa karibu sana.Ametokea wapi huyu jamaa? Gosu Gosu aliuliza

“Again,jielekeze katika kazi uliyokuja kuifanya,usitake kujua zaidi” alisema Jombaa

“Nataka kufahamu mpango mzima wa kumuondoa huyu jamaa”

“Kama ulivyoelekezwa kazi hii inakwenda kufanyika usiku wa leo.Huyu jamaa tumekuwa tukifuatilia nyendo zake tangu alipokuja Arusha tumegunuda kwamba kila siku saa mili za usiku huenda katika sehemu ya chakula katika hoteli alikofikia.Baada ya kupata chakula hupumzika kwa muda kidogo akipata kinywaji huku akiburudika na muziki wa bendi.Hutumia dakika chache kisha hurejea chumbani

kwake.Wakati akipata chakula wewe utaingia chumbani kwake utajificha.Atakaporejea chumbani ndipo utakapommaliza.” Jombaa alimpa Gosu Gosu maelekezo. Baada ya majadiliano mafupi Gosu Gosu alipelekwa katika chumba alichoandaliwa ndani ya ile nyumba nzuri.Alikaa kitandani akainamisha kichwa akazama mawazoni.

“Hawa watu ni akina nani? Huyu jamaa anayetakiwa kuuawa ni nani na amefanya nini? Alijiuliza

“Maswali ni mengi ya kujiuiliza na itanichukua muda kupata jibu la hiki kilichotokea hadi nimefika hapa nilipofika.Nikiwa ndegeni nimetafakri mno jambo hili sijalipatia majibu.Nini hasa kilitokea usiku ule hadi nikajikuta nimefanya mapenzi na Elizabeth? Nisiumize sana kichwa changu kwa sasa,ngoja kwanza niwafanyie kazi yao halafu nitalifuatilia suala hili hadi niupate ukweli.Hata hivyo natakiwa kuwa makini mno kwa sababu tayari hawa jamaa wanaonekana ni

mtandao mkubwa.” Aliwaza na kuvua viatu akajilaza kitandani

“Wamefahamuje historia yangu? Wamefahamuje kama mimi ninaweza kuwasaidia katika kazi yao? Imenishangaza sana.Lakini nitafahamu kila kitu baada ya kukamilisha kazi yao.Suala hili siwezi kuliacha likapita hivi hivi lazima lichunguzwe kwa undani sana” aliwaza Gosu Gosu na kuamua kujilaza kitandani akisubiri muda ufike ili akatekeleze kile kilichompeleka Arusha

KONGWA HOTEL

Gosu Gosu akiwa ameongozan na Jombaa,waliwasili Kongwa hotel.Kulikuwa na magari kadhaa eneo la maegesho na mengi kati ya magari hayo yalikuwa ni yale magari yanayotumika kubeba watalii.Walishuka garini wakaelekea hotelini.Walipita mapokezi wakaelekea kwa moja moja upande wa chakula.Kulikuwa na watu wengi wakipata chakula h.Akina Gosu Gosu walitafuta

sehemu wakaketi wakaagiza chakula.

Macho ya Jombaa hayakutulia sehemu moja.Aliyazungusha kama Kinyonga akijaribu kumsaka yule mtu wanayemtafuta.Wakati wakiendelea kupata chakula ujumbe ukaingia katika simu ya Jombaa akausoma halafu akamtazama Gosu Gosu

“Jamaa tayari ameshuka.Kazi inaanza” alisema Jombaa.Gosu Gosu aliyekuwa amevaa suruali ya

jeans ya bluu na koti jeusi huku kichwani akiwa na kofia pana iliyomfanya asionekane vizuri sura yake,aliinuka akaelekea chumba no 73.Hakuonekana kuwa na wasi wasi wowote.

Alikifikia chmba no 73,akatoa mfukoni kadi ya kufunguilia mlango aliyopewa na Jombaa.Kabla hajaipitisha katika mlango alitoa glovu akavaa mikononi kisha akaipitisha mlangoni ile kadi halafu akakinyonga kitasa akaufungua mlango akaingia ndani.Macho yake yalitua

katika meza ya kusomea kulikokuwa na kompyuta mpakato.Alielekea mezani iliko kompyuta akaigusa ikawaka.

“Inaonekana huyu jamaa alikuwa anaendelea na kazi akaamua kushuka mara moja kwenda kupata chakula halafu arejee kuja kuendelea na kazi zake ndiyo maana akaiacha kompyuta yake katika hali hii.’ Aliwaza Gosu Gosu.Pale mezani aliziona diski mweko mbili.

“Natakiwa kujua huyu jamaa ni nani” aliwaza Gosu Gosu huku akiichukua diksi mweko moja akaichomeka katika ile kompyuta akaitazama akakuta ina nafasi ya kutosha akaanza kuhamisha mafaili kutoka katika kompyuta kwenda katika ile diski mweko.Wakati mafaili yakiendelea kuhama aliichukua kamera iliyokuwa pale mezani akatoa kadi ya kuhifadhia picha akaiweka mfukoni. Aliufungua mlango wa kabati la nguo lakini kabla hajafanya chochote alisikia

vyuma vya kitasa vikiachia ishara kwamba mlango unafunguliwa.Kwa kasi ya aina yake Gosu Gosu aliruka hatua mbili kubwa na kujificha nyuma ya mlango.Mlango ulifunguliwa jamaa mmoja aliyevaa kaptula ya khaki na fulana nyeupe akaingia.

Mara tu alipoufunga mlango alikutana na kitu ambacho hakuwa amekitegema.Mtu mmoja mwenye sura ya kikatili alikuwa amesimama nyuma ya mlango akimtazama.

“Shit ! alisema yule jamaa na kunyoosha mkono wake ili kukishika kitasa kwa lengo la kuufungua mlango lakini mguu wenye kasi ya ajabu wa Gosu Gosu uliupiga ule mkono kisha ngumi nzito ikatua katika paji la uso wa yule jamaa akaenda chini.Salamu ile ilimpa picha yule jamaa kuwa mvamizi wake ni hatari sana na asipofanya jitihada anaweza kuuawa. Aliuinua mkono wake ili aiguse meza ndogo iliyokuwa na chungu cha maua lakini macho ya Gosu Gosu yaliona kama

Tai,aliruka teke zito lilimpata jamaa usoni akaanguka chini akagonga kichwa sakafuni kwa kishindo.Gosu Gosu aliruka juu huku ameukunja mguu wake wa kulia na kutua juu ya kifua cha yule jamaa ambaye alitoa mgumo wa maumivu makali.Gosu Gosu hakumpa nafasi alimsindikiza na ngumi mbili nzito za haraka haraka.Kwa mikono yake yenye nguvu Gosu Gosu alimkaba koo yule jamaa ambaye alijaribu kujinasua lakini mikono ya Gous Gosu ilikuwa migumu kama chuma

na taratibu jamaa alianza kuishiwa pumzi.Baada ya muda alinyooka hakuwa na uhai tena.Gosu Gosu alimtazma kwa makini kujiridhisha kuwa kweli amekufa.Alipojiridhisha yule jamaa kweli amekufa alimvuta na kumuweka bafuni.Alimpekua akamkuta na simu.Aliifungua simu ile akaitoa laini na kadi ya kumbu kumbu halafu akaivunja vunja ile simu kisha akavichukua vile vipande akaenda kuvitupa chooni.Aliiendea tena kompyuta,tayari ilikwisha

maliza kuhamisha mafaili akaichomoa ile diski mweko akaificha.Kutoka mfukoni akatoa kitu Fulani alichopewa na Jombaa akakibonyeza .Baada ya dakika mbili mlango ukagongwa akaenda kufungua akamkuta Jombaa na kijana mwingine ambao waliingia ndani haraka haraka

“Kila kitu tayari” alisema Gosu Gosu na kuwaonesha mwili wa yule jamaa uliokuwa bafuni.Waliuhakiki kama kweli amekufa halafu wakaichukua kompyuta na kamera vilivyokuwa mezani.Jombaa

alienda kumpekua yule jamaa lakini hakupata kile alichokuwa anakitafuta

“Huyu jamaa hana simu? Aliuliza lakini hakuna aliyemjibu.Alimpekua tena lakini hakuipata simu akaenda katika kabati la nguo akalipekua lakini hakuiona simu.Alilifunua godoro lakini hakuipata simu.

“Tusipoteze muda.Kama angekuwa na simu tungekwisha iona.Chukueni vile vilivyopo tuondoke.Tunaweza kukutwa

humu na mambo yakabadilika” alisema Gosu Gosu

“Lazima niipate simu yake ni muhimu sana.” Alisema Jombaa

“Inaonekana hana simu huyu mtu kama angekuwa nayo mngekwisha ipata” alisema Gosu Gosu.

Jombaa aliendelea kupekua sehemu mbali mbali akiitafuta simu ya yule jamaa bila mafanikio.Alisimama akashika kiuno hakuamini kama ameikosa

simu.Alitafakari kwa muda halafu akachukua simu yake akampigia mtu wakazungumza kwa sekunde kadhaa halafu akaikata ile simu akawataka waondoke mle ndani.Walichukua kile walichokipata wakaondoka.

Walifika katika makazi yao na mara tu baada ya kuingia ndani Gosu Gosu akamtaka Jombaa ampigie simu mkuu wao ili azungume naye

“Brother utazungumza na mkuu baaada ya kumaliza kazi aliyokutuma uje kuifanya hapa

Arusha” alisema Jombaa.Gosu Gosu alimtazma kwa macho makali sana ya kikatili

“Nimetoka kuondoa uhai wa mtu usiku huu kwa kutumia mkono yangu.Sishindwi kuondoa uhai wako na hao wakuu wako.Sitaki kuingia katika matatizo na ninyi tafadhali naomba umpigie simu mkuu wako nizungumze naye! Alifoka Gosu Gosu.Jombaa ambaye alikuwa na tabasamu lililojaa ukatili aliingiwa na hofu

“Huyu jamaa si wa kufanyia masihara.Anaonekana ni mtu katili mno” aliwaza Jombaa akaitoa simu mfukoni mwake akapiga halafu akampa Gosu Gosu

“Jombaa” ilisema suti ya mwanamke baada ya kuipokea simu

“Unazungumza na Gosu Gosu.”

“Unasemaje Gosu Gosu?

“Nimemaliza kazi ya kwanza uliyonituma nije

kuifanya hapa Arusha.Lini kazi nyingine ya mwisho itafanyika?Kumbuka makubaliano yetu yalikuwa ni kuja kufanya kazi mbili tu.” Alisema Gosu Gosu

“Gosu Gosu kazi ya mwisho itafanyika kesho kutwa usiku.Utapewa maelekezo na Jombaa kesho jioni” alisema Bernadetha

“Sawa” alisema Gosu Gosu na kukata simu akamgeukia Jombaa

“Nimeambiwa kazi ya mwisho itakuwa kesho

kutwa.Usiku huu nahitaji kwenda klabu nzuri hapa Arusha yenye wanawake warembo” alisema Gosu Gosu

“Brother maelekezo niliyopewa ni kuhakikisha hautoki humu ndani.Kila unachokihitaji tutakuletea hapa hapa.Kama shida ni kinywaji au mwanamke vyote utavipata hapa hapa.Utatoka nje ya nyumba hii pale utakapokuwa unakwenda kutekeleza kazi ulizotumwa kuja kuzifanya.Hii ni kwa ajili ya usalama wako” alisema

Jombaa.Gosu Gosu alitoa kicheko kidogo halafu alisema

“Jombaa inaonekana wewe na wakuu wako bado hamjanifahamu vyema mimi ni mtu wa aina gani.Kwa ufupi tu mimi ni mtu katili mno.Sitishwi na sipangiwi nini cha kufanya.Tafadhali sitaki matatizo yoyote nawe.Nipeleke katika klabu nzuri ya usiku hapa Arusha yenye makahaba wazuri.Nahitaji mtoto mzuri wa kupitisha naye usiku wa leo.Nimetoka kutoa uhai wa mtu kwa kutumia mikono yangu hivyo nahitaji kuliondoa

tukio lile katika akili yangu.Tafadhali nipeleke klabu ila usimwambie mkuu wako.Vile vile naomba pesa taslimu za matumizi” alisema Gosu Gosu.Jombaa alifikiri kidogo

“Sawa brother nitakupeleka.Unahitaji kiasi gani?” alisema Jombaa

“Milioni tatu”

“Milioni tatu? Jombaa alishangaa

“Ndiyo ninaomba kiasi hicho.Usijali nitakaporejea Dar

es salaam nitakurejeshea pesa yako” alisema Jombaa

“Pesa yote hiyo ni kwa ajili ya kutumia usiku wa leo na makahaba? Jombaa aliuliza

“Ndiyo.Ni pesa kidogo sana hiyo.Fanya juu chini uipate tafadhali” alisema Gosu Gosu huku akipiga hatua kuelekea chumbani kwake akakaa kitandani.

“Yule mtu niliyetoa uhai wake ni nani? Hawa watu ni akina nani? Wanatafuta nini kwa yule mtu? Kwa nini wamemuua? Kwa nini

waliihitaji sana simu yake?.Hawa watu ni hatari sana na ninapaswa kuwa mwangalifu.Wanaonekana ni mtandao mkubwa na wenye nguvu.” Alitolewa mawazoni baada ya mlango kufunguliwa.Alikuwa ni Jombaa ambaye mkononi alikuwa ameshika suruali ya jeans iliyopauka,fulana nyeupe na koti.

“Naamini hizi nguo zinaweza kukutosha” alisema Jombaa

“Ahsanate Jombaa lakini sihitaji mavazi.Vipi kuhusu fedha nilizokuomba umezipata? Aliuliza Gosu Gosu

“Sijafanikiwa kuzipata zote nimepata milioni mbili pekee”

“Zinatosha hizo” alisema Gosu Gosu.Jombaa akampatia zile fedha.

“Usihofu fedha zako zote zitarudi” alisema Gosu Gosu.Bila kuzihesabu zile fedha aliziweka mfukoni.

Dakika chache baadaye waliondoka kuelekea katika

klabu ya usiku kama alivyoomba Gosu Gosu

****

Eneo la kuegesha magari katika klabu ya usiku ya Alinde iliyoko katikati ya jiji la Arusha lilifurika magari.Jombaa aliegesha gari na kumgeukia Gosu Gosu

“Hii ni klabu maarufu sana hapa Arusha inaitwa Alinde night club.Kila starehe unayoitaka iko humu ndani.Nataka uniambie saa

ngapi nje nikuchukue? Aliuliza Jombaa

“Nitakuwepo hapa hadi asubuhi.Nikimaliza starehe zangu nitakuja mwenye huna haja ya kunifuata” alisema Gosu Gosu. Akafungua mlango akashuka.Aliangaza angaza pale maegesho halafu akaanza kupiga hatua kuelekea ndani ya klabu.Aliingia upande wa baa akachagua meza iliyokuwa sehemu yenye mwangaza hafifu akaketi.Haraka haraka muhudumu alifika Gosu Gosu akaagiza bia.Aliletewa kinywaji akaendelea kunywa taratibu

huku akiyachunguza mazingira ya pale ndani.Nje ya baa kulikuwa na ujia ambao watu walikuwa wakipita wakionekana kuelekea sehemu Fulani.Gosu Gosu alimuita muhudumu akamuuliza kama kulikuwa na ukumbi mwingine pale akaambiwa kuna ukumbi wa disko ulioko chini ya ardhi.Gosu Gosu alitabasamu akampa muhudumu noti moja ya shilingi elfu kumi kama ahsante akainuka akaenda katika dirisha ambako watu walikuwa wanakata tiketi kwa ajili ya kuelekea ndani ya

ukumbi wa disko.Alikata tiketi akafuata njia inayoelekea katika ukumbi wa disko chini ya ardhi.Tiketi yake ilikaguliwa akaingia ndani.Kulikuwa na watu wengi wakicheza muziki.Wengine walikuwa katika sehemu za kupumzikia wakipata vinywaji.Gosu Gosu alienda kaunta akanunua kinywaji akaenda kuketi katika sofa nzuri akaanza kuangaza angaza akiwatazama watu waliokuwa wanacheza muziki.Taratibu aliinuka akapanda ngazi kuelekea sehemu ya juu ili aweze

kutazama vizuri kinachoendelea ndani ya ule ukumbi.

Akiwa juu aliangaza chini akawaona wanawake watatu wakiwa wametulia katika moja ya kona ya ukumbi wakionekana ni makahaba walio katika mawindo yao.Hakukawia, alimuita muhudumu mmoja wa kiume akampatia noti ya shilingi elfu kumi akamtaka akawaite wale wanawake watatu.Hawakukataa haraka haraka walipanda juu na kumkuta Gosu Gosu

akawakaribisha katika meza yake.

“Karibuni warembo.Kabla ya yote kila mmoja wenu aagize kile anachotaka kutumia” alisema Gosu Gosu.Wanawake wale waliokuwa wamevalia nusu utupu walitabasamu na muhudumu akaitwa mara moja wakaagiza kila mmoja kile alichokihitaji.

“Nimewaona kule chini mko peke yenu nikaamua kuwaita huku juu ili tuburudike kwa

pamoja.Tumekuja hapa kuburudika hivyo hampaswi kuwa wapweke.Kila mmoja ajisikie huru kutumia kile anachokihitaji" alisema Gosu Gosu huku akitabasamu

"Tunashukuru sana kaka kwa ukarimu wako.Lakini wewe nani mwenzetu? Ni nadra sana kukutana na mtu mkarimu kama wewe zama hizi." Aliuliza mmoja wa wale wadada wazuri

"Naitwa John Mbuji ni mfanya biashara wa madini" alisema Gosu Gosu

“Ouh ! karibu sana mimi naitwa Witney,mwenzangu pale anaitwa Sakina na yule pale ni Mima” alisema Witney mwenye sauti laini na mwili mwembamba.Alionekana kuwa mstaarabu zaidi kuliko wenzake waliokuwa wanakunywa pombe kwa fujo.

Walizungumza mambo mengi huku vinywaji vikijaa mezani kila pale vilipopungua.Baada ya kuona wanawake wale wamekwisha lewa Gosu Gosu aliinuka akawapatia Sakina na Mima

kila mmoja shilingi laki moja akaondoka na Witney.

“Umekuja na gari? Aliuliza Witney ambaye alionekana kuzidiwa na kinywaji

“Tutachukua taksi.” Alisema Gosu Gosu akamshika mkono Witney wakaelekea upande ziliko taksi.

“Niwapeleke wapi kaka? Aliuliza dereva wa taksi

“Nataka unipeleke katika hoteli yenye hadhi hapa jijini.” Alielekeza Gosu Gosu.Dereva

aliondoa gari wakaikata mitaa kadhaa ya jiji la Arusha.

Walifika Kobe hotel moja ya hoteli nzuri ya kitalii jijini Arusha wakapata chumba katika ghorofa ya nne.Kilikuwa ni chumba kizuri kikubwa kilichokamilika kila kitu ndani

“Kaka agiza kinywaji tuendelee kunywa” alisema Witney.

“Hapana.Kinywaji ulichokunywa kinatosha sana.Kwa sasa nataka tuzungumze” alisema Gosu Gosu

“Tuzungumze? Ulinileta hapa tuzungumze? Kama ni mazungumzo tumeshazungumza kule baa.Hapa tumekuja kwa kazi moja tu ya kustarehe” alisema Witney

“Usihofu kuhusu kustarehe.Ninachohitaji kwanza ni kufahamiana.Nahitaji kukufahamu nawe pia unahitaji kunifahamu.” Alisema Gosu Gosu

“Nimekwisha jitambulisha kwako ninaitwa Witney.Nini

unataka kukifahamu zaidi? Hebu achana na hayo mambo nikustareheshe nawe unipe changu nijikatae” alisema Witney.Gosu Gosu alimtazama akauliza

“Witney kuna kitu nataka kukuuliza,naomba unijibu tafadhali”

“Unataka kuuliza nini? Aliuliza Witney

“Katika hii biashara unayoifanya unaingiza kiasi gani kwa siku? Aliuliza Gosu Gosu

“Kwa nini unataka kujua?

“Wajihi wako haufanani kabisa na biashara hii.Uko tofauti na wenzako wote”

“Kaka unadhani wote wanaofanya biashara hii wanapenda? Ni shida kaka yangu ndizo zinazopelekea tukafanya hii biashara.Ni mateso matupu hakuna tunachokipata.Kwa sasa biashara imekuwa ngumu mno,wateja hakuna.Ukipata hata wa kukununulia bia moja unashukuru.Unaweza ukamaliza hata wiki nzima

hujapata mwanaume wa kutoka naye” alijibu Witney

“Biashara inapokuwa nzuri huwa unapata kasi gani kwa siku? Gosu Gosu aliuliza

“Hakuna kiwango maalum.Unaweza ukaondoka na laki moja mbili au hata tano kama ukipata mzungu.Mbona unataka sana kufahamu kipato changu? Aliuliza Witney

“Ni kwa sababu ninataka kukusaidia”

“Kunisaidia vipi we kaka? Aliuliza Witney

“Ninataka kukusaidia kukuondoa katika hii biashara unayoifanya.Kama nilivyokwambia awali kwamba wajihi wako haufanani kabisa na hii kazi unayoifanya ya kuuza mwili” alijibu Gosu Gosu

“Ni vipi unataka kunisaidia?

“Kwanza nataka kujua kiwango chako cha elimu kama hutojali”

“Niliishia kidato cha pili nikapata ujauzito nikafukuzwa shule.Wazazi wangu

walinifukuza nyumbani.Niliishi maisha ya shida sana hadi nikalazimika kuingia katika hii biashara ya kuuza mwili”

“Mwanao yuko wapi? Aliuliza Gosu Gosu

“Alifariki akiwa na miaka miwili” alijibu Witney

“Pole sana”

“Ahsante.Yote haya niliyataka mwenyewe kwa kuwapuuza wazazi walionitaka nisome niachane na masuala ya mapenzi shuleni” alisema

Witney akainamisha kichwa alionekana kuzama mawazoni

“Witney ahsante kwa kunieleza historia yako.Waswahili wanasema yaliyopita si ndwele tugange yajayo.Kwa sasa jielekeze katika kutengeneza kesho yako iwe nzuri kuliko leo” alisema Gosu Gosu

“Ah ! aliguna Witney

“Mimi nimekwisha kata tamaa na maisha yangu ndiyo maana nimeamua kuingia barabarani kujiuza” alisema Witney.Kimya kifupi kilipita

“Ikitokea mtu anataka kukusaidia upate kazi,ni kazi ipi ungependelea kuifanya?

“Sina elimu na siwezi kupata kazi yoyote ya maana.Halafu kipato cha kusubiri hadi mwisho wa mwezi nitashindwa”

“Sikiliza Witney.Ninataka kukusaidia kukuondoa katika haya maisha unayoishi sasa lakini ninahitaji ushirikiano wako” alisema Gosu Gosu

“Unataka kunisaidiaje? Aliuliza Witney

“Ninataka kukusaidia kupata kazi ya maana yenye staha ili uweze kuondokana na maisha haya unayoishi sasa.Nataka uwe na ajira ya kudumu,uwe na uhakika wa kupata fedha hata kama ni mwisho wa mwezi kuliko kazi hii unayoifanya” alisema Gosu Gosu

“Kazi gani unataka kunisaidia kuipata? Kama nitaona inanifaa basi nitaifanya”

“Witney kwa sasa wewe si wa kuchagua kazi.Yoyote ile

ambayo itapatikana wewe ifanye lakini ninachoweza kukuahidi ni kwamba kazi yoyote ile utakayoipata iwe ndogo au kubwa malipo yake yatakuwa manono sana”

“Haya nakusikiliza.Mbona hutaki kuniambia hiyo kazi yenyewe ni ipi? Aliuliza Witney

“Mimi ni mkurugenzi wa kampuni inayojishughulisha na usindikaji wa maziwa jijini Dar es salaam.Nitampa maelekezo mtu Fulani ambaye

utakwenda kuonana naye kesho.Je uko tayari?

“Unataka niende Dar es salaam? Aliuliza Witney

“Ndiyo.”

“Mimi nimezoea sana Arusha,huko Dar es salaam sipawezi”

“Utapaweza tu.Ninaomba simu yako” alisema Gosu Gosu.Witney alifungua pochi yake kubwa akatoa pochi nyingine ndogo akaifungua na kutoa simu ndogo akampatia Gosu Gosu.Aliandika namba

akapiga halafu akafungua mlango akatoka nje ya kile chumba.

“Hallow ” ilisema sauti ya upande wa pili baada ya kuipokea ile simu

“Mathew ni mimi Gosu Gosu”

“Gosu Gosu ! kulikoni hupatikani simuni? Kuna tatizo gani?

“Sikiliza Mathew nimekuja Arusha lakini hakuna anayejua.”

“Kuna nini huko Arusha?

“Mathew sina muda mrefu lakini .....” hakumaliza sentensi yake simu ikakatika.Muda wa maongezi ulikwisha.Mara tu alipogeuka ili arudi ndani Mathew alipiga

“Gosu Gosu kuna tatizo gani?

“Kuna mtu ninamtuma kwako kesho, atakuja na ndege ya asubuhi utampokea.Nitampa ujumbe muhimu sana akuletee.Ukiupokea ujumbe huo ufanyie kazi haraka sana.Mtu huyo nitakayemtuma

anahitaji kazi hivyo msaidie aweze kupata kazi”

“Sawa Gosu Gosu.”

“Thank Mathew” alisema Gosu Gosu akakata simu akarejea chumbani akamkuta Witney ameingia bafuni anaoga.Alisogea katika mlango wa bafu akajiridhisha kuwa anaoga halafu akanyata hadi katika pochi ya Witney akaifungua akakuta kuna mipira sita ya kiume nguo ya ndani ,suruali na fulana.Vile vile kulikuwa na mswaki,dawa ya mswaki,chupa ndogo ya

uturi na fulana.Katika mfuko mdogo uliokuwa ndani ya pochi alikuta kitambulisho cha taifa na laini tatu za simu akaichukua laini moja halafu akaifunga ile pochi.

Mlango wa bafu ulifunguliwa Witney akatoka akiwa amejifunga taulo.

“Nilihisi joto na uchovu nikaenda kuoga.Sasa najihisi vizuri” alisema Witney huku akiliachia taulo alilojifunga lianguke akabaki mtupu.Gosu Gosu alihisi kudondokwa na mate alipoushuhudia mwili

mwororo wa Witney.Aliifungua pochi yake akatoa nguo ya ndani nyeupe akavaa halafu akaenda kujilaza kitandani.

“Tayari nimempa maelekezo mtu wangu utakwenda kuonana naye kesho asubuhi na ikiwezekana kesho hiyo hiyo utaanza kazi” alisema Gosu Gosu.Witney aliyekuwa amejilaza kitandani akainuka

“Umesema kesho asubuhi?

“Ndiyo kesho asubuhi.Utaondoka na ndege

ya saa kumi na mbili asubuhi” alijibu Gosu Gosu

“Ndege? Aliuliza Witney

“Ndiyo utaondoka na ndege” alijibu Gosu Gosu na kumfanya Witney aangue kicheko

“Haya mbona makubwa.Miye wa kujiuza nitatoa wapi hela ya kulipia ndege? Aliuliza

“Usihofu nitakulipia nauli” alisema Gosu Gosu akaenda katika simu ya mezani iliyokuwamo mle chumbani

akapiga simu huduma kwa wateja pale hotelini akawajulisha kuwa anahitaji huduma ya fedha.

“Unataka kufanya nini? Aliuliza Witney

“Ninataka kuweka hela katika simu yako ili ninunue tiketi ya ndege”

“Hivi ni kweli unamaanisha unachokisema?Witney aliuliza

“Ndiyo nina maanisha”

“We kaka sikuelewi.Nimekutana nawe

usiku huu,mara hii hii unataka kunilipia nauli ya ndege niende Dar kufanya kazi? Haya mbona maajabu”

“Si maajabu Witney.Hii ni bahati imekuangukia” alijibu Gosu Gosu na mlango ukagongwa.Witney alijifunika shuka .Gosu Gosu aliufungua mlango akakutana na muhudumu akamtaka amuwekee katika ile simu kiasi cha shilingi milioni moja.Witney alibaki anashangaa hakuamini.Pesa iliwekwa katika simu,muhudumu akaondoka

zake.Bila kupoteza muda Gosu Gosu alipiga simu ofisi za shirika la ndege kuulizia kama angepata nafasi moja katika ndege ya saa kumi na mbili asubuhi inayoelekea Dar es salaam.Alifanikiwa kupata tiketi.Bado Witney alikuwa kwenye mshangao asiamini kile kilichokuwa kinatokea

“Mambo yamekwisha.Kesho asubuhi utasafiri na ndege kwenda Dar,utapokelewa uwanja wa ndege wa Julius Nyerere .Ikiwezekana kesho hiyo hiyo

utaanza kazi” alisema Gosu Gosu

“Mbona mambo haya yanakwenda haraka namna hii? Mbona hakuna maandalizi? Nitaishi wapi huko Dar? Nitakula nini? Nitavaa nini? Witney aliuliza

“Kwanza kabisa utakapoondoka hapa Arusha sahau kabisa kila kitu chako.Kule Dar utapewa nyumba ya kuishi,utapata kila unachokihitaji.Witney hii si ndoto,hiki ni kitu cha kweli kabisa

kinakutokea.Unakwenda kubadilisha maisha yako.Bahati kama hizi hutokea mara chache sana hivyo nakusihi itumie bahati hii" alisema Gosu Gosu

"Nitaaminije kama haya yote unayonieleza ni ya kweli? Nitaaminije kama kweli wewe ni mmiliki wa kampuni huko Dar es salaam?

"Witney mimi nimejitolea kukusaidia kukuondoa katika maisha haya unayoishi sasa.Ni juu yako kuniamini au kutokuniamini.Kama uko

tayari, tuendelee na hatua inayofuata” alisema Gosu Gosu

“Sawa nitakwenda lakini…”

“Ahsante kwa kukubali.Sasa vaa nguo twende katika duka la mavazi tukanunue mavazi utakayovaa wakati ukiondoka Arusha” alisema Gosu Gosu .Witney alivaa suruali yake iliyokuwa kwenye pochi na fulana wakashuka chini ambako kulikuwa na duka kubwa linalofunguliwa kwa saa ishirini na nne.Witney

alichagua mavazi aliyoyataka halafu wakarudi chumbani

“Kaka hivi wewe ni mtu kweli au ni malaika? Witney aliuliza

“Kwa nini?

“Haya mambo uliyonifanyia sikuyategemea kabisa ndiyo maana ninakuona wewe kama si binadamu wa kawaida.”

“Usihofu Witney mimi ni binadamu wa kawaida kabisa.Ninakusaidia kwa sababu hata mimi niliwahi kusaidiwa hadi nikafika hapa

nilipofika” alijibu Gosu Gosu huku Witney akijaribu mavazi aliyonunuliwa.Alipomaliza Gosu Gosu alimpa bahasha ya khaki

“Jamaa unayekwenda kukutana naye anaitwa Mathew.Utampa hii bahasha.”

“Kuna nini ndani ya hiyo bahasha? Aliuliza witney

“Tafadhali usiifungue bahasha hii.Hakikisha umempatia muhusika mwenyewe” alisema Gosu Gosu.Witney aliiweka vizuri

bahasha ile.Kilichofuata baada ya hapo ni mtanange mkali.

****

Gosu Gosu alirejea kutoka uwanja wa ndege wa Kilimanjaro alikomsindikiza Witney kupanda ndege kuelekea Dar es salaam.Alimtaka dereva wa taksi aliyopanda amrejeshe katika hoteli alikolala.Kabla ya kwenda chumbani kwake aliingia katika supermarket kubwa ya pale hotelini akanunua simu akaenda nayo

chumbani.Aliichaji simu ile kwa dakika chache halafu akaiweka ile laini aliyoichukua kwa Witney.Uliingia ujumbe mwingi lakini hakuujali akaandika namba ya simu ya Mathew akampigia

“Hallow” alisema Mathew

“Mathew, Gosu Gosu hapa naongea.”

“Gosu nini kinaendelea? Kwa nini hutumii namba yako ya simu? Aliuliza Mathew

“Mathew, tayari mtu niliyemtuma yuko angani hivi

sasa anakuja Dar es salaam.Nimempatia bahasha akuletee.Ina vitu vya muhimu sana.Laini ya simu,kadi za kumbu kumbu ya simu na kamera pia diski mweko" alisema Gosu Gosu

"Gosu Gosu tafadhali naomba uniweke wazi kuhusu kile kinachoendelea.Hivyo vitu unavyovileta kwangu umevitoa wapi? Vina umuhimu gani? aliuliza Mathew

"Mathew siwezi kuingia kwa undani zaidi.Nitakueleza kwa undani zaidi

nitakaporejea Dar es salaam.Kwa ufupi tu ili upate picha ni kwamba hivyo vifaa nilivyovituma kwako ni vya mtu ambaye nimeletwa kuja kumuua hapa Arusha”

“Umepelekwa kuua mtu Arusha? Nani amekupeleka huko? Aliuliza Mathew kwa mshangao mkubwa

“Mathew kwa sasa naomba niishie hapo kwani kazi bado inaendelea.Nitakaporejea Dar es salaam nitakueleza kwa undani zaidi kile kinachoendelea hapa

Arusha.Ninataka umpatie Ruby vifaa hivyo nilivyovituma kwako avichunguze ili nimfahamu mtu yule niliyemuua ni nani.Nataka nijue kwa nini ilikuwa lazima auawe? Alisema Gosu Gosu

“Gosu Gosu umeingia katika hatari kubwa sana.Tafadhali kuwa makini na hicho ulichokwenda kukifanya.Kuwa makini sana kuanzia sasa ili hao waliokutuma ufanye mauaji hayo wasigundue kitu ulichokifanya.Kama kuna watu wamekupeleka huko Arusha

kufanya mauaji basi watu hao hawawezi kukuacha hai baada ya kumaliza kazi yao.” alisema Mathew

“Ahsante Mathew.Nitakupigia simu baadae kwa sasa ninakwenda kuonana na hao watu ili kujua kile kinachoendelea.Nitakupigia simu baada ya kutoka huko.Mathew naomba jambo hili libaki siri yako asifahamu Ambola wala mtu mwingine yeyote kama niko Arusha” alisema Gosu Gosu akaagana na Mathew

“Lazima nimfahamu mtu yule ni nani na kwa nini akauawa.Lazima ipo sababu iliyopelekea akauawa. Bado picha ya mama yake Ambola inanijia kichwani.Je Ambola anafahamu kama mama yake ni mkatili kiasi hiki? Bado natafakari kuhusu tukio la siku ile usiku.Ilikuaje nikajikuta katika chumba na mdogo wake Ambola? Kuna maneno alitamka Ambola kwamba mapenzi niliyompa usiku ule alihisi kama amehamia sayari nyingine.Je ni mimi ndiye niliyefanya naye mapenzi au

kuna mwanaume mwingine aliyefanya naye mapenzi? Kwa nini mdogo wake Ambola hakuonekana kushtushwa na kitendo cha mimi kurekodiwa nikifanya naye mapenzi? Nini kinaendelea hapa? Alijiuliza Gosu Gosu

Aliizima simu akaiacha katika chaji akatoka na kwenda mapokezi akalipia kile chumba kwa simu mbili zaidi halafu akachukua taksi kuelekea katika makazi ya Jombaa.

“Yule Jombaa ana macho ya kikatili sana.Anaonekana ni muuaji.Kwa nini walishindwa kumtumia kumuua yule jamaa hadi wakanitafuta mimi? Taarifa zangu zote wanazo, walizipataje? Aliendelea kujiuliza Gosu Gosu akiwa garini akirejea katika makazi ya Jombaa.

Taksi aliyopanda ilimfikisha mahali alikotaka akamlipa dereva halafu akaelekea katika geti akausukuma mlango mdogo pembeni ya geti akaingia ndani.Gari la Jombaa lilikuwemo mle ndani.Moja

kwa moja alienda katika mlango wa mbele akagonga.Mlango ulifuguliwa Gosu Gosu akaingia ndani.Aliwakuta watu sita wakichambua bangi.Aliwasalimu wakamkaribisha akawajulisha kuwa hatumii kilevi kile.Moja kwa moja alielekea katika chumba chake

“Usiku wako ulikuaje? Aliuliza Jombaa aliyemfuata Gosu Gosu chumbani

“Ulikuwa mzuri.Sikutegemea kama hapa

Arusha kungekuwa na klabu nzuri kiasi kile” alisema Gosu Gosu,Jombaa akatabasamu

“Ulifanikiwa kupata kahaba wa kupitisha naye usiku wa jana?

“Niliwapata watatu” alijibu Gosu Gosu

“Uliwatumia wote watatu?

“Wote watatu,sikuacha hata mmoja” alijibu Gosu Gosu

“Kuwa makini na wanawake wa Arusha.Watakuputisha fedha zote”Jombaa alitoa tahadhari

“Starehe gharama.” Alijibu Gosu Gosu akamfanya Jombaa atabasamu

“Kuna mabadiliko yoyote kuhusiana na kazi ya mwisho ninayotakiwa kuifanya kesho ? Aliuliza Gosu Gosu

“Hapana hakuna mabadiliko yoyote.Kila kitu kitakwenda kama kilivyopangwa” alijibu Jombaa

“Sawa.Ninaomba nipumzike.Sijalala usiku kucha” alisema Gosu Gosu na Jombaa akageuka ili aondoke

“By the way,hakuna tatizo lolote kuhusiana na ile kazi ya jana? Aliuliza Gosu Gosu

“Usiwe na hofu yoyote.Wewe maliza kazi uliyopewa mengine hayakuhusu” alijibu Jombaa akafunga mlango akatoka.

DAR ES SALAAM

Simu ya Mathew Mulumbi iliita ikiwa ni ile ile namba ambayo aliitumia Gosu Gosu usiku.Tayari Mathew alikuwa uwanja wa ndege wa kimataifa

wa Dar es salaam akimsubiri mgeni wake kutoka Arusha.

“Hallow” alisema Mathew baada ya kuipokea simu

“Kaka habari yako” ilisema sauti ya mwanadada

“Salama.Nani mwenzangu? Mathew aliuliza

“Ninaitwa Witney nimetokea Arusha nimeelekezwa kwako.”

“Umekwisha fika Dar es salaam? Mathew aliuliza

“Ndiyo nimekwisha fika.Tayari nimetoka nje ya

uwanja wa ndege” alijibu yule mwanamke.Mathew alimpa maelekezo mahali alipo.Baada ya dakika chache yule mwanamke tayari alifika mahali aliko Mathew ambaye alikuwa garini akimsubiri

“Shikamoo kaka” alimsalimu yule dada

“Marahaba.Natumai wewe ndiye mgeni wangu” alisema Mathew

“Ndiyo” alijibu yule mwanamke

“Karibu sana Dar es salaam” alisema Mathew akampokea sanduku lake akaliweka garini akamfungulia mlango akaingia ndani wakaondoka

“Wewe ndiye Mathew? Aliuliza yule mgeni

“Ndiyo.” Alijibu Mathew

“Nimetumwa kwako na John Mbuji”

“Amekwisha nieleza kila kitu kuhusu wewe hivyo usihofu ,kila kitu kitakwenda kama alivyokuahidi” alisema

Mathew safari ikaendelea kimya kimya.

“Lini umefahamiana na John? Aliuliza Mathew

“Nilikutana naye katika mihangaiko ya maisha.Ni mtu mzuri sana aliamua kunisaidia”

“Kuna mzigo wowote alikupa unipatie?

“Ndiyo.” Alijibu Witney

Safari iliishia nyumbani kwa Ruby.Mathew alishuka akamfungulia Witney mlango akashuka wakaingia

ndani.Ruby alikuwepo nyumbani akimsubiri Mathew na mgeni wake.Aliwakaribisha sebuleni

“Ruby huyu ndiye mgeni wetu anaitwa Witney.” Mathew alifanya utambulisho mfupi

“Karibu sana Witney” alisema Ruby

“Ahsante sana dada Ruby”alisema Witney.

“Witney kabla hatujaendelea naomba unipatie ule mzigo wangu

uliopewa na John.” Alisema Mathew.Witney alifungua sanduku lake akatoa bahasha akampatia Mathew

“Ahsante sana.Maelekezo niliyopewa na John ni kwamba unatafuta kazi” alisema Mathew

“Ndiyo kaka”

‘VIzuri.Kazi umeipata.Dereva atakupeleka mahali utakapoanza kufanya kazi kuanzia kesho.Utapata sehemu ya kuishi katika nyumba za wafanyakazi .Kazi utakayoanza kuifanya ni

kufanya usafi katika ofisi za viongozi,vile vile kuwahudumia kwa chakula n.k.Utapewa maelekezo utakapofika huko sehemu ya kazi.Hiyo ni kazi utakaoanza nayo lakini mshahara wake utakuwa mkubwa kwani umepewa upendeleo maalum.Baada ya kuajiriwa utapatiwa mafunzo ya kompyuta kisha utaanza kuifanya kazi za ofisi.Kwa chochote kile utakachohitaji usisite kuwasiliana nami moja kwa moja nitakusaidia” alisema Mathew na kufungua

pochi yake akahesabu kiasi cha shilingi laki tano akampatia Witney kwa ajili ya kuanzia maisha yake Dar.

Dereva wa Ruby alimchukua Witney na kumpeleka katika kampuni ya kusindika maziwa ambayo Gosu Gosu ni mkurugenzi wake.Mara tu Witney alipoondoka Mathew aliifungua ile bahasha aliyopewa, ndani yake alitoa laini ya simu na kadi mbili za kuhifadhi kumbu kumbu.Moja ikiwa ni kadi ya kamera na nyingine ya simu pamoja na

diski mweko.Ruby ambaye tayari alikwisha dokezwa na Mathew kuhusiana na Gosu Gosu,alizipokea kadi zile moja kwa moja wakaelekea katika ofisi yake ya nyumbani.Aliingiza ile laini ya simu katika kifaa kilichounganishwa na kompyuta yake na kazi ya kuanza kusaka taarifa za kuhusiana na ile laini ya simu ilianza mara moja.Mathew alikuwa pembeni akamuacha Rubyu autumie utaalamu wake wa udukuzi .Baada ya dakika tano Ruby alimgeukia Mathew.

“Hii laini imesajliwa kwa jina la Anganile Mwaikusa.Ana miaka ishirini na saba ni dereva.” Alisema Ruby na kumuonesha Mathew picha ya mtu ya Anganile Mwaikusa.Mathew akaitazama kwa makini

“Kwa nini ameuawa huyu kijana? aliuliza

Ukimya ulipita kila mmoja akitafakari.Baada ya muda Ruby aliendelea na zoezi lake

“Kuna kitu kinashangaza Mathew.Hii laini ina namba moja tu iliyohifadiwa.Hii ina

maana huyu jamaa alikuwa anawasiliana na mtu mmoja pekee” alisema Ruby

“Inashangaza.Au alikuwa na laini nyingine ambayo alikuwa anaitumia kwa mawasiliano.Hata hivyo laini hii kuwa na namba moja pekee inaonesha hii laini ilikuwa na upekee kwa huyu mtu.Unaweza ukajua ni namba ya nani iliyohifadhiwa katika hiyo laini? Aliuliza Mathew.Ruby aliendelea kubonyeza kompyuta kama vile ana vidole sita kila

mkono.Baada ya muda mfupi alishtuka

“Kuna nini Ruby? Mathew aliuliza

“Namba iliyomo katika hii laini inaonesha ni ya mtu anaitwa Jackson Igaya Mzumile” alijibu Ruby

“Una hakika? Mathew aliuliza

“Ndiyo Mathew.Huyu ni Gavana wa benki kuu” alisema Ruby

“Inashangaza sana.Huyu mtu alikuwa anawasiliana na

Gavana? Unaweza ukapata kumbu kumbu za mawasiliano yao tujue walizungumza nini? Aliuliza Mathew.

“Itanilazimu kuingia katika hifadhi za mtandao wa simu” alisema Ruby

“Kuna ugumu wowote kwako wa kuingia huko? Mathew aliuliza.Ruby alicheka kidogo halafu akasema

“Mathew ni muda mrefu hatujafanya kazi, unaonekana umeanza kunisahau uwezo wangu katika masuala haya ya udukuzi.Haya ni mambo

madogo sana kwangu” alisema Ruby

“Siwezi kukusahau Ruby.Uwezo wako ni wa kipekee sana katika kucheza na mtandao” alisema Mathew.Ilimchukua dakika saba Ruby kupata mazungumzo ya mwisho ya Anganile na Gavana Jackson .Mazungumzo yao yalikuwa mafupi sana na walitumia lugha ya kiingereza.

“Hallo Peter” ilisema sauti ya Gavana

*“Mzee nimefika salama Arusha na tayari nimeanza kazi yangu”*alisema Anganile

“Vizuri sana.Utakapoimaliza kazi yako utanijulisha.Usinipigie simu mara ka mara hadi pale utakapokuwa umeikamilisha kazi yako au pale utakapokuwa na jambo zito ” alisema Gavana

“Nimekuelewa mzee”

“Vizuri.Nakukumbusha usihofu kutumia fedha katika ile akaunti kila pale utakapokuwa na uhitaji wa

fedha” alisema Gavana na kukata simu.

“Haya mawasilino yalifanyika wiki tatu zilizopita.” Alisema Ruby

“Kwa muda wa wiki hizo tatu Anganile na Gavana hawakuwasiliana tena.Hii inanipa picha kuwa huyu mtu alitumwa na Gavana kwenda Arusha kwa kazi maalum na kwa muda huu wote hakuwa ameikamilisha kazi aliyotumwa ndiyo maana hakumpigia simu Gavana.Swali la kujiuliza je ni

kazi hiyo aliyutumwa kuifanya ndiyo iliyopelekea akauawa? Ni kazi gani hiyo? Aliuliza Mathew

“Bado sipati picha kwa nini akauawa kwa sababu huyu mtu kazi yake ni dereva.Angeuawa na watu wengine tungehisi labda ni majambazi ambao walitaka kumpora fedha.Lakini aliuliwa na Gosu Gosu ambaye anadai alitumwa kwenda kufanya mauaji hayo.Kuna kitu hapa” alisema Ruby

“Nakubaliana nawe ipo sababu nzito.Kuna kitu kingine nimekipata katika yale mazungumzo.Huyu mtu jina lake ni Anganile lakini Gavana alimuita Peter.Je ana majina mawili? Tuliweke pembeni hilo tukague hivi vitu vingine.Tuanze na hii diski mweko” alisema Mathew

Ruby aliichomeka diski mweko katika kifaa maalum akaanza kupitia mafaili yaliyokuwamo ndani yake ambayo Gosu Gosu aliyatoa katika ile kompyuta ya mtu aliyemuua.Ruby alianza

kuyapitia mafaili yale haraka haraka,Mathew aliinuka akaenda maliwato.Baada ya dakika tatu akarudi

“Kuna chochote umekipata? Aliuliza

“Hakuna vitu vingi katika haya mafaili.Nilichofanikiwa kukipata ni video nane ngoja tuzitazame” alisema Ruby wakaanza kuzitazama video zile.Zote zilimuonesha mwanamke mmoja mzuri mwenye umbo zuri akiwa mtupu chumbani.Video ya kwanza ilimuonesha

mwanamke yule akiwa anajipaka mafuta baada ya kutoka bafuni kuoga,alijitazama katika kioo akatabasamu.Video nyingine zilimuonesha mwanamkeyule katika nyakati mbali mbali na zote akiwa mtupu.

“Hizi video zinaonesha zilichukuliwa bila huyu mwanamke kujua kama anachukuliwa.Inaonesha zilitoka katika kamera ya siri iliyofngwa katika nyumba chake” alisema Ruby

“She’s very hot.Nadhani ndiyo maana huyu jamaa hakuzifuta video hizi ili aweze kuzitazama mara kwa mara” alisema Mathew

“Nawe tayari umekwisha anza kutamani.Acha hayo mambo Mathew” alisema Ruby akiendelea kupitia mafaili mengine

“Kuna faili lingine linaonesha alikuwa anafanya rekodi ya kitu.Inaonesha muda wa kuamka,muda wa kujiandaa,muda wa kuondoka.Sina hakika kama

hii ilikuwa ratiba yake ya siku au vipi lakini amrekodi kwa siku kumi na saba hadi tarehe ya jana.Katika faili lingine kuna picha za watu kadhaa.Faili hili lina kichwa “ALIOKUTANA NAO”

“Katika hizi kadi za kumbukumbu kuna nini? Aliuliza Mathew.Ruby aliziingiza zile kadi katika kifaa maalum.Kadi ya simu ilikuwa na miziki michache .Kadi ya kamera ilikuwa na picha kadhaa.Walizipitia zote zilikuwa za mwanamke mmoja

“Huyu mwanamke ndiye yule ambaye ameonekana mtupu katika zile video” alisema Mathew.

“Ni mwenyewe.Unapata picha gani Mathew? Aliuliza Ruby

“Picha ninayoipata hapa kuna kitu kinaendelea kati ya Anganile na huyu mwanamke.Anazo video nane zikimuonesha huyu mwanamke akiwa mtupu.Ukiacha video hizo anazo picha nyingi za mwanamke yule yule katika

kamera yake hii inaonesha kuna kitu baina yao”

“Kingine ninachokiona katika hizi picha zilipigwa kwa kuibia.Si picha ambazo zilipigwa huku muhusika akijua kama anapigwa picha” alisema Ruby wakaendelea kuzichunguza zile picha

“Nakubaliana nawe picha hizi zilipigwa bila muhusika kufahamu.” Aliongeza Mathew

“Nilikuambia hata zile video zilichukuliwa bila mhusika kujua.Inaonesha wazi zilichukuliwa kutoka katika

kamera za siri pia” alisema Ruby

“Tujiulize swali,kwa nini? Aliuliza Mathew

“Swali lingine je kifo chake kina mahusiano yoyote na huyu mwanamke? Je huyu mwanamke ni nani? Tukifahamu huyu mwanamke tunaweza kupata kitu hapa” Alisema Mathew.Ruby aliichukua picha ya yule mwanamke akaiingiza katika program ya utambuzi wa sura.Baada ya dakika moja

programu ikampata yule mwanamke

“Anaitwa Regina William Zanga.Ana miaka 31.Ni mwanasheria kitaaluma.Kwa sasa anajishughulisha na siasa.Ni naibu katibu mkuu wa chama cha siasa cha Ukombozi wa Afrika.” alisema Ruby

Kilipita kimya cha dakika mbili.

“Ruby hili suala si dogo.Kuna utata mkubwa hapa.Inanilazimu niende Arusha.Huko ndiko kuna majibu.Sababu nyingine Gosu

Gosu atakuwa katika hatari kubwa.Aliponipigia simu aliniambia amepelekwa kwenda kumuua huyu Anganile.Hii ina maana hajakwenda kwa ridhaa yake.Nani amempeleka huko akafanye mauaji?.Nina uhakika baada ya kumaliza kazi aliyotumwa kuifanya hao jamaa watamuua ili waendelee kuificha siri yao.Gosu Gosu ni mkurugenzi wa makampuni,ana fedha nyingi na hana sababu ya kufanya mauaji kwa malipo.Lazima ipo sababu nzito iliyompelekea

akakubali kwenda Arusha kufanya mauaji.Gosu Gosu ni mwenzetu lazima kufanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha tunamtoa katika hatari aliyomo.Ni yeye ndiye atakayetufumbua macho kuhusu suala hili.”alisema Mathew.

“Mathew nitaongozana nawe kwenda Arusha kumsaidia Gosu Gosu” alisema Ruby

“Hapana Ruby.Bado hatuwafahamu watu hawa ni akina nani na nguvu yao ni.....”

Mathew alitaka kusema kitu. Ruby alimkatisha

“Mathew tusiweke mjadala katika suala hili.Gosu Gosu ni mwenzetu.Sisi ni familia moja hivyo mwenzetu anapokuwa katika tatizo lazima wote tushirikiane kumtoa katika tatizo.Tunakwenda wote Arusha.Tumefanya kazi nyingi nimekwisha komaa hivi sasa siogopi tena mikiki mikiki.” Alisema Ruby.

“Sawa.Tutakwenda wote.” alisema Mathew na mara moja wakaanza maandalizi

ARUSHA

Ilipata saa kumi na moja jioni pale Gosu Gosu alipoamka.

“Nahitaji kurejea kule hotelini.Nataka kuwasiliana na Mathew nijue kama tayari wamemfahamu yule jamaa”aliwaza Gosu Gosu akaingia bafuni akaoga halafu akamfuata Jombaa aliyekuwa sebuleni akisafisha bastola zake

“Kuna mabadiliko yoyote kuhusiana na kazi iliyobaki?aliuliza

“Hakuna mabdiliko yoyote.Kazi itafanyika kesho kama ilivyopangwa.” Alijibu Jombaa

“Vizuri sana.Mimi ninaondoka tutaonana hiyo kesho”

“Unakwenda wapi? Hutakiwi kuonekana mitaani ni hatari kwako”

“Ninakwenda ile klabu ulikonipeleka jana.Siwezi kukaa hapa kama ninatumikia adhabu.Nahitaji mwanamke wa kuniliwaza usiku wa leo.Nipeleke pale tafadhali”

alisema Gosu Gosu.Jombaa alifikiri kwa muda.

“Sawa nitakupeleka” alisema

Baada ya dakika chache waliondoka kuelekea Alinde night club.

“Unajishughulisha na mambo gani hapa Arusha? Gosu Gosu alimuuliza Jombaa wakiwa garini

“Nilikutahadharisha toka jana kuwa maliza kazi uliyotumwa kuja kuifanya

uondoke.Mambo mengine hayakuhusu” alijibu Jombaa

“Sorry” alisema Gosu Gosu safari ikaendelea kimya kimya hadi walipofika Alinde club

“Leo utarudi au utalala club? Jombaa aliuliza

“Usiku wa leo sintarudi” alijibu Gosu Gosu

“Kama utalala club basi kesho asubuhi na mapema urejee nyumbani kwa sababu maandalizi ya kazi ya kesho yataanza asubuhi” alisisitiza Jombaa

“Nitajitahidi usihofu” alijibu Gosu Gosu huku akishuka garini

“Nakuonya tena kuwa mwangalifu sana unapojichanganya na makahaba” alisema Jombaa.Gosu Gosu hakumjali.Aliufunga mlango wa gari akaanza kutembea mwendo wa taratibu kuelekea ndani ya klabu.Jombaa aligeuza gari akaondoka.

Aliingia klabuni akapanda sehemu ya juu akaangaza ngaza halafu akamuomba

muhudumu akamuitie mwanadada mmoja mfupi mweupe aliyekuwa ameketi kitini akionekana kusubiri kuitwa.Mwanadada yule alifika kwa haraka.Gosu Gosu aliongea naye huku wakipata vinywaji.Hayakuwa mazungumzo marefu walielewana halafu wakatoka wakaeleka mahali zinakoegeshwa taksi .Gosu Gosu alimuelekza dereva awapeleke katika hoteli nzuri yenye utulivu.

Dakika tatu baada ya kuondoka pale klabuni,Gosu

Gosu akamtaka dereva asimamishe gari.Alitoa bunda la noti akamuhesabia yule mwanamke kiasi cha shilingi laki moja akampatia

“Nimekumbuka kuna sehemu muhimu sana ninahitajika hivi sasa.Nakuja kukutafuta tena kesho.Samahani kwa kukusumbua” alisema Gosu Gosu.Yule mwanadada alishangaa kupewa fedha zile bila kazi yoyote.Alishukuru akashuka garini ,dereva akaondoa gari.Gosu Gosu alimuelekeza dereva ampeleke

katika ile hoteli alikokuwa amekodisha chumba

“Kaka mbona umemuacha yule mtoto? Aliuliza dereva

“Nilikuwa nimesahau kama nina kikao muhimu sana usiku wa leo.Kama nitawahi kumaliza kikao nitarudi kumtafuta” alijibu Gosu Gosu

Alifikishwa katika hoteoli alikokuwa amekodi chumba.Alimlipa dereva akaingia ndani.Alipita mapokezi akapewa funguo yake akaeleka chumbani.Kitu cha kwanza alichokifanya

baada ya kuingia chumbani ni kuiwasha simu.Uliingia ujumbe mwingi hakuujali kwani laini ile ya simu haikuwa yake.Moja kwa moja aliandika namba ya simu ya Mathew akampigia.Simu iliita ikapokelewa

“Hallow” ilisema sauti ya Mathew Mulumbi

“Gosu Gosu hapa ninaongea”

“Imekuwa vyema umepiga.Tulikuwa na wasi wasi sana namna ya kuweza kukupata”

“Mathew mnaendelaje huko ? Mgeni alifika salama? Aliuliza Gosu Gosu

“Mgeni alifika salama.Amenikabidhi mzigo uliomtuma”

“Mmeufanyia kazi tayari? Kuna chochote mmekipata? Aliuliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu mimi na Ruby tayari tuko hapa Arusha.Uko wapi hivi sasa? Tunahitaji kuonana nawe” alisema Mathew na kumshtua sana Gosu Gosu

“Mmekuja Arusha?

“Ndiyo.Tuko hapa Arusha.Tuelekeze ulipo tafadhali tunahitaji kuonana nawe.Kama mazingira hayaruhusu mahali ulipo basi tuelekeze tukutane wapi? Aliuliza Mathew

“Mathew nimeshtuka sana,sikutegema kabisa”

“Gosu Gosu tutazungumza zaidi tukionana.” Alisema Mathew.Gosu Gosu aliwapa maelekezo wafike pale Kobe hotel.

****

Mathew na Ruby walifika katika hoteli aliko Gosu Gosu na kwa kuwa walikwisha elekezwa namba ya chumba hawakusumbuka kuuliza mapokezi moja kwa moja walielekea katika chumba cha Gosu Gosu.Mathew aligonga mlango wa chumba ukafunguliwa,Gosu Gosu alibaki anashangaa

“Uliponiambia kuwa mko hapa Arusha sikuamini kabisa.” Alisema Gosu Gosu

akiwa bado amesimama akishangaa

“Usijali Gosu Gosu.Tunashukuru sana kukuona tena ukiwa mzima” alisema Mathew

“Mmefika saa ngapi? Aliuliza Gosu Gosu

“Tumefika jioni hii.Hapa ndipo ulikofikia? Una hakika ni salama? Mathew aliuliza

“Nilifikia katika nyumba fulani.Hapa hotelini nilifika jana usiku nikachukua hiki chumba ukiwa ni mpango

wangu wa kutaka kuwafikisha vile vifaa.Kutwa nzima ya leo nimeshinda na hao jamaa.Usiku huu nikawaambia kuwa ninahitaji kutoka kupunga upepo na kutafuta mwanamke wa kuniliwaza ndipo nikaja hapa”

“Una hakika uko salama? Hawajui chochote kuhusiana na wewe kupanga chumba katika hii hoteli? Aliuliza Mathew

“Hapana hawafahamu chochote.Hivi sasa wanaamini

niko klabu ninastarehe na makahaba” alijibu Gosu Gosu

“Good.” Alisema Mathew na kuvua koti lake akalitundika ukutani

“Karibuni sana jamani.Kinywaji gani mtatumia?

“Gosu Gosu huu ni wakati wa kazi.Kinywaji baadae.” Alisema Mathew na kumtazama Gosu Gosu

“Kwanza kabisa pole sana Gosu Gosu kwa matatizo yaliyokufika.Tutazungumza

baadae kujua nini kinachoendelea hapa lakini kwa sasa nataka tuzungumze kuhusiana na yule mtu ambaye ulitutumia vifaa vyake.”alinyamaza tena kidogo halafu akampa ishara Ruby aendelee

“Yule mtu anaitwa Anganile Mwaikusa.Ana miaka 27.Kabila ni Mnyakyusa.Kazi ni dereva.Ile laini ya simu uliyoituma ina namba moja tu ambayo baada ya kuichunguza tuliigundua ni ya Gavana wa benki kuu.Tulifanikiwa kupata mazungumzo yao ya mwisho”

alisema Ruby na kucheza yale mazungumzo ya Gavana na Anganile.Gosu Gosu aliyasikiliza vyema halafu Ruby akaendelea

“Katika diski mweko tulikuta kuna video kadhaa za utupu za mwanamke ambaye baada ya kumchunguza tumemfahamu kuwa ni Regina William Zanga.Ana miaka 31.Ni mwanasheria na kwa sasa ni naibu katibu mkuu wa chama cha siasa cha Ukombozi wa Afrika” Ruby alimuonesha Gosu Gosu video zile.

“Katika kadi ya kumbu kumbu ya simu hatukupata chochote cha maana zaidi ya miziki.Katika kadi ya kamera tumekuta kuna picha nyingi za mwanamke yule anayeonekana katika zile video.” Alimaliza Ruby akamtazama Mathew

“Uchunguzi wetu unaanzia hapo.” Alisema Mathew akatoa faili katika mkoba wake akalifungua na kutoa picha tatu akaziweka mezani

“Hapa tuna watu watatu.Anganile,Gavana na Regina” alisema Mathew na

mara Gosu Gosu akashtuka baada ya kuziona zile picha.Aliishika picha ya Anganile

“Huyu ni nani? Aliuliza

“Huyu ndiye yule mtu uliyetutumia vifaa vyake.Ndiye Anganile Mwaikusa” alijibu Mathew

“Hapana” alisema Gosu Gosu na kuiweka mezani ile picha

“Huyu siye yule niliyemuua.Huyu ni mtu tofauti kabisa” alisema na

chumba kikawa kimya.Baada ya muda Mathew aliuliza

“Gosu Gosu una uhakika kweli huyu siye yule uliyemuua?

“Ndiyo Mathew.Huyu siye yule niliyemuua” alijibu Gosu Gosu

“Inawezekanaje? Ile laini ya simu uliyoituma imesajiliwa kwa kutumia kitambulisho cha huyu mtu unayemuona pichani” alisema Ruby

“Lakini siye niliyemuua’ alisisitiza Gosu Gosu.Baada ya

sekunde chache Mathew alisema

“Kuna uwezekano akawa anatumia laini ya mtu mwingine?

“Hilo linawezekana kabisa.Yawezekana alikuwa anatumia laini iliyosajiliwa na huyu Anganile.” Alijibu Ruby

“Kama ndiyo,kwa nini? Aliuliza Gosu Gosu

“Hapo ndipo tunapotakiwa kuanzia kutafuta majibu kwa nini atumie namba iliyosajiliwa kwa jina la mtu

mwingine? Je hakutaka kufahamika? Kama hakutaka kufahamika kitu gani alichokuwa anakifanya kibaya hadi ajifiche katika mgongo wa mtu mwingine?.Kuna ulazima wa kuipata sura ya huyo mtu aliyeuawa halafu tumtafute na kumfahamu Anganile ni nani na kwa nini kitamblisho chake kimetumika kusajili laini ya simu ya huyu jamaa.Baada ya hapo tutamchunguza Gavana kwani ndiye aliyewasiliana na huyu mtu na kwa mujibu wa mazungumzo yao inaonekana kama vile huyu mtu alitumwa

kazi na Gavana” alisema Mathew

“Kitendo cha kukutwa na laini ambayo haijasajiliwa kwa jina lake kinaleta mashaka” alisema Gosu Gosu

“Tukirudi upande wa pili tujiulize kwa nini ameuawa? Hapo ndipo tunaporudi kwako Gosu Gosu utueleze kisa kizima hadi umefika Arusha ukafanya yale mauaji.” Alisema Mathew

Gosu Gosu alikohoa kidogo halafu akaanza kuwasimulia akina Mathew

kisa kzima kilichotokea siku ile ya sherehe ya kuzaliwa kwa mpenzi wake Ambola.Aliwaeleza kila kitu bila kuwaficha chochote.Ruby alibaki katika mshangao mkubwa baada ya kusikia kile kilichotokea katika ile sherehe.

“Gosu Gosu hicho ni kisa cha kweli kilikutokea wewe au ni ndoto uliota? Aliuliza Ruby

“Ni kitu cha kweli kabisa kilitokea na hata mimi hadi leo bado najiuliza namna jambo lile lilivyotokea” alisema Gosu Gosu

“Mhh ! aliguna Ruby

Gosu Gosu aliendelea kuwasimulia kile kilichofuata baada ya tukio lile kutokea.Alieleza alivyokutana na mama yake Ambola hotelini akamlazimisha kufanya mapenzi.”

“Ulifanya nini Gosu Gosu? Aliuliza Ruby huku akimtazama Gosu Gosu kwa sura yenye mshangao

“Alinilazimisha sikuweza kukataa.Alikuwa na video yangu nikifanya mapenzi na mtoto wake ambaye ni

mwanafunzi na alitishia kunifikisha polisi kama ningekataa kufanya kile ambacho angeniamuru kukifanya”

“Hata hivyo Gosu Gosu hukupaswa kumkubalia.Unadhani mpenzi wako akisikia kitu kama hicho nini kitatokea?

“Ruby naomba unielewe sikuwa na namna yoyote ya kukataa.Yule mama tayari alikuwa ameshika mpini.Ningewezaje kusema hapana wakati nje kulikuwa na

gari la askari wakisubiri amri tu wanikamate? Ukiacha ile video tayari alikuwa amejenga hoja kuwa nimempa mimba mtoto wake na tayari ushahidi wa hospitali ulikwisha tengenezwa.Ungekuwa ni wewe ungefanya nini? Aliuliza Gosu Gosu.Ruby hakujibu kitu

“Endelea Gosu Gosu” alisema Mathew.Gosu Gosu alieleza kuwa baada ya kufanya mapenzi na yule mama ndipo alipopewa kazi ya kwenda Arusha kwenda kuua watu wawili.

“Hivyo ndivyo ilivyokuwa ndugu zangu.Kitanzi tayari kilikwisha fungwa shingoni hivyo sikuwa na namna ya kujiokoa zaidi ya kukubali kufanya kile wanachokitaka hawa watu.Nililetwa Arusha na usiku wa jana nikamuua yule jamaa.Kwa bahati nzuri nilifanikiwa kupata vile vifaa nikavituma kwenu.”alisema Gosu Gosu

“Pole sana Gosu Gosu.Hili ni jambo zito .Inaonesha hawa jamaa walianza kukuchunguza kwa muda mrefu hadi wakafanikiwa kupata taarifa

zako zote halafu wakatengeneza lile tukio ili kukulazimisha ufanye kazi yao.Dhumuni letu la kuja hapa ni kuhakikisha unakuwa salama kwani hao jamaa baada ya kuwafanyia kazi yao hawatakuacha salama.Lazima watakuua ili kuendelea kuificha siri yao.Nina swali kwako.Una hakika Ambola hafahamu chochote kuhusiana na lile tukio la wewe kulala na mdogo wake? Mathew aliuliza

“Hapo ndipo ninapochanganyikiwa kwa sababu nilipoingia chumbani

kwa Ambola asubuhi alinisifu kwa gwaride nililomchezesha usiku ule.Sikumbuki kama nilifanya naye mapenzi usiku ule.Nahisi hafahamu chochote.” alijibu Gosu Gosu

“Tuliweke pembeni hilo kwanza.Nataka kufahamu mtu wa pili ambaye umeletwa kuja kumuua na mpango mzima wa mauaji ukoje? Aliuliza Mathew

“Mpaka sasa bado hawajaniambia nani ambaye ninakwenda kumuua ila mauaji hayo yatafanyika kesho”

“Hawajakueleza yatafanyikia wapi? Aliuliza Mathew

“Hapana hawajanieleza.Maelekezo yote nitayapata kesho”

“Sawa.Kuna mambo mawili ambayo tunatakiwa kuyafanya kwa usiku hu.Kwanza ni kumchunguza zaidi huyu Anganile.Tunahitaji kumfahamu kiundani halafu tutafute mahusiano yake na huyu marehemu.Tumekwisha wafahamu nani waliohitaji huyu jamaa afe hivyo moja

kwa moja tunaanza kuichunguza familia ya Ambola hasa mama yake ambaye ndiye aliyesimamia mchakato mzima wa kumleta Gosu Gosu hapa Arusha ili amuue yule jamaa.”alisema Mathew

“Anaitwa nani mama yake Ambola? Aliuliza Ruby

“Ninamfahamu kwa jina lake moja tu la Bernadetha.Ambola aliwahi kunitajia majina yake ila nimeshau ninalikumbuka hilo

moja tu la Bernadetha. Alijibu Gosu Gosu

“Hakuna tatizo endelea kumfuatilia huyo Anganile sisi ngoja tukafuatilie tuipate picha ya yule jamaa aliyeuawa.” Alisema Mathew

Walimuacha Ruby mle chumbani wakaondoka kuelekea hospitali kuu ya mkoa wa Arusha.

“Mathew mtanisamehe nimewasumbu sana hadi mmekuja huku.Hata mimi sikutegemea kabisa kama

yangenikuta mambo haya.”Alisema Gosu Gosu

“Usijali Gosu Gosu sisi ni ndugu na wakati wote lazima tusimame pamoja pale mmoja wetu anapokuwa katika matatizo.”Alisema Mathew.Walikuwa wanatembea kwa mguu kuelekea katika kituo cha taksi

“Mathew suala hili unalionaje? Aliuliza Gosu Gosu

“Mapema sana kusema chochote kwa sasa kuhusiana na suala hili ila lazima tulichunguze kwa undani

tufahamu kwa nini watu hao wawili wanatakiwa kuuawa? Jambo lingine kwa nini wakakuchagua wewe uwaue watu hao na si mtu mwingine? Wapo watu wengi ambao wangewez a kuifanya hiyo kazi lakini kwa nini wakawekeza nguvu na fedha hadi wakakuweka katika mikono yao?

“Hilo suala hata mimi nimejiuliza sana kwa nini mimi? Hapa Arusha wana watu wao ambao ukiwaona unajua dhahiri ni watu wa kazi.Kiongozi wao anaitwa

Jombaa ana macho ya kikatili sana.” Alisema Gosu Gosu

“Ndiyo maana nikasema suala hili ni pana zaidi hivyo inabidi tulichunguze kwa undani kabisa na kwa umakini mkubwa.” Alisema Mathew

“Vipi kuhusu huyo mtu ambaye ninatakiwa kumuua kesho? Aliuliza Gosu Gosu

“Imekuwa bahati mbaya mpaka sasa haijajulikana ni nani anayetakiwa kuuawa.Hata hivyo lazima tutafute namna yoyote ya kumuokoa mtu huyo ili

asiuawe.Huyo mtu anaweza akatusaidia kufahamu kwa nini anatakiwa kuuawa”

“Nadhani hiyo itatusaidia sana kufahamu kwa nini watu hawa wanatakiwa kuuawa.” Alisema Gosu Gosu

“Tutalijadili hilo tutakaporejea.” Alisema Mathew wakati wakiingia katika uzio wa ukumbi mmoja wa burudani ambako kulikuwa na taksi kadhaa zimeegeshwa zikisubiri abiria.Walichukua taksi na kuelekea hospitali ya rufaa ya mkoa ya Mount Meru.

****

Mlango wa chumba alichopanga Gosu Gosu katika hoteli ya Kobe uligongwa.Ruby ambaye alibaki chumbani mle akiendelea na kazi aliinuka akaufungua mlango kwa tahadhari kubwa.Alishusha pumzi baada ya kuwaona Mathew na Gosu Gosu

“Karibuni tena.” Alisema Ruby

“Mambo yanakwendaje hapa? Aliuliza Mathew huku akilitundika koti lake ukutani

“Nimeifanya ile kazi.Nimemchimba Anganile nimegundua ana namba nyingine mbili za simu alizozisajili kwa jina lake”alisema Ruby

“Good.Sisi pia tumefanikiwa kuupata mwili wa yule jamaa.Umehifadhiwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa na mpaka sasa hakuna ndugu yeyote aliyejitokeza kuutambua mwili huo.Tumeipiga picha sura yake.” Alisema Mathew na kumuonesha Ruby picha ya yule jamaa.

“Unadhani tunaweza kupata taarifa zake kwa kutumia sura hii? Aliuliza Mathew

Ruby aliitazama na kusema

“Nitajaribu kutafuta picha inayofanana nayo”

“Good fanya hiyo kazi.” Alisema Mathew.Ruby aligeukia kompyuta yake akaanza kazi.

Zilipita dakika tano akatikisa kichwa

“Hakuna picha yoyote inayofanana na huyu mtu”

“Tumekwama” alisema Gosu Gosu

“Gosu Gosu hao watu unaoshirikiana nao hawawezi wakakueleza huyu mtu ni nani na kwa nini akauawa? Aliuliza Ruby

“Nimejaribu kuwadadisi inaonekana hata nao hawafahamu chochote” alijibu Gosu Gosu

“Vipi kama tukimteka mmoja wao tukambana

korodani unadhani hatasema huyu mtu ni nani? Aliuliza Ruby

“Tukitumia njia hiyo tutazidi kumuweka Gosu Gosu katika hatari.Kuna kitu ninakifikiria.” Alisema Mathew

“Kitu gani? aliuliza Ruby

“Huyu Anganile bandia alikuwa na picha za yule mwanamke Regina.Hamuhisi labda wawili hawa wana mahusiano Fulani?

“Hilo la mahusiano mimi ninalipinga kwa sababu kama

wangekuwa na mahusiano tungekuta namba ya yule mwanamke katika laini yake ya simu lakini mle tulikuta namba moja tu ya Gavana.Pile ni aina ya uchukuaji wa zile picha.Kama nilivyokueleza jana kuwa picha zile zinaonesha zimechukuliwa bila mlengwa kujua kama anachukuliwa picha.Hata zile video zinazomuonesha Regina akiwa mtupu zinaonesha zilichukuliwa katika kamera za siri bila mwenyewe kufahamu.Kama wangekuwa na mahusiano sina hakika

kama angempiga picha kwa siri.” Alisema Ruby na kuwatazama akina Mathew.Alifungua folda ambalo alikuwa amezihifadhi zile picha za Regina.

“Ukizichunguza picha hizi kwa makini sana utagundua asilimia kubwa ya picha zote mpigaji alikuwa ndani ya gari.” Alisema Ruby huku akifungua picha moja baada ya nyingine kuthibitisha kile alichokisema

“Je huyu jamaa alikuwa anamfuatilia Regina?” aliuliza Gosu Gosu

“Inaonekana hivyo ,huyu jamaa alikuwa anamfuatilia Regina.Kama hivyo kwa nini?” aliuliza Ruby

“Ukifuatilia mzungumzo ya Anganile bandia na Gavana tunapata picha Fulani.Huyu jamaa alimjulisha Gavana kuwa tayari amekwisha fika Arusha na ameianza kazi.Gavana alimtaka kutumia kiasi chochote cha fedha katika akaunti ili aweze kuikamilisha kazi.Je kazi aliyotumwa ni kumfuatilia Regina? Kama ndiyo kwa nini? Je huyu jamaa ni mpelelezi? aliuliza Mathew

“Nimekumbuka kitu.Katika moja ya faili tulilolipata kutoka katika kompyuta ya Anganile bandia lilionesha ratiba” alisema Ruby na kulifungua lile faili.Wote wakalisoma

“Hii inaonesha ni ratiba aliyokuwa anajaza kila siku.Tukiacha hili faili kuna faili ingine lina kichwa cha habai Aliokutana nao.Ndani yake kuna picha za watu mbali mbali .Ninahisi hawa watu ambao ameweka picha zao walikutana na Regina.” Alisema Ruby

“Kuna uwezekano mkubwa huyu jamaa alikuwa anamfuatilia Regina.Kwa nini alikuwa anamfuatilia? Ni Gavana ndiye aliyemtuma? Majibu halisi tungeweza kuyapata kutoka kwa muhsika mwenyewe ambaye hayupo duniani hata hivyo ni wajibu wetu kutafuta majibu.Ninadhani bado kuna ulazima wa kukutana na Regina kumchunguza kujua kama anamfahamu huyu mtu na kwa nini hasa anafuatiliwa.”alisema Mathew

“Ni wazo zuri.” Alisema Gosu Gosu

“Kazi inayokuja mbele yetu kwa sasa ni kumsaka Regina kujua mahali alipo.Ruby ifanye kazi hiyo ili hadi kesho asubuhi tuwe na taarifa zake zote muhimu.Gosu Gosu kwa usiku huu nadhani tumemaliza hivyo wewe utarejea katika makazi ya hao akina mjomba” alisema Mathew Gosu Gosu akacheka kidogo

“Anaitwa Jombaa.” Alisema Gosu Gosu

“Sawa utarejea huko kwa akina Jombaa ila utavaa saa maalum ambayo itakuwa ni kwa ajili ya mawasiliano kati yako na sisi.Utakapobonyeza moja ya kitufe tutaweza kusikia kila kitu mahali ulipo.Kuna laini la simu humo ndani ambayo utaitumia katika kuwasiliana nasi.Kupitia saa hiyo tutaweza kujua mahali ulipo,unakoelekea na kila kinachoendelea hivyo basi hata pale utakapokuwa katika hatari itakuwa rahisi kwetu kufahamu na kutafuta namna

ya kukusaidia kwa haraka.Kesho jitahidi kwa namna yoyote ile utujulishe ni nani ambaye anatakiwa kuuawa.Ukimfahamu utatujulisha mara moja mahali alipo ili tufanye taratibu za kumuokoa na kupitia kwake tufahamu kwa nini anatakiwa kuuawa" alisema Mathew

"Sawa Mathew.Nitarejea katika makazi ya wale jamaa,nitajitahidi kuwachunguza zaidi na pindi tu nitakapofahamu ni nani ambaye anatakiwa kuuawa

kesho nitawajulisha.” Alisema Gosu Gosu.

Baada ya mikakati kadhaa waliondoka katika kile chumba,Gosu Gosu akielekea katika makazi ya akina Jombaa huku akina Mathew wakielekea katika hoteli walikofikia.

****

Mlango mdogo wa geti katika makazi ya akina Jombaa haukuwa umefungwa.Gosu

Gosu aliusukuma akaingia ndani moja kwa moja alielekea katika mlango mkuu wa sebuleni akagonga.Alifunguliwa mlango akaingia sebuleni ambako aliwakuta jamaa wawili wamekaa wakitazama runinga.Aliwasalimu akajiunga nao.

“Tayaru umekuwa mwenyeji wa jiji la Arusha” alisema mmoja wao

“Nimewahi kufika Arusha wakati fulani.Ni jiji

zuri.Nilitoka kwenda kutafuta mtoto wa kiarusha”

“Mbona umerejea mapema sana? Sisi tulijua hutarudi leo”

“Nimechoka.Nimeamua kurudi kuja kupumzika nikisubiri kazi ya kesho.Jombaa yuko wapi? Aliuliza Gosu Gosu

“Jombaa ametoka amekwenda katika mizunguko yake” alijibu mmoja wa wale jamaa

“Mnatumia kinywaji gani? aliuliza Gosu Gosu huku akitoa

kitita cha noti akahesabu shilingi laki mbili akaziweka mezani

“Leteni vinywaji tuendelee kubudurika hapa ndani” alisema Gosu Gosu.Wale jamaa wakajadiliana halafu mmoja wao akachukua zile fedha wakatoka.Ulisikika muungurumo wa gari baada ya dakika chache mmoja wa wale jamaa akarejea ndani.

“Ahsante brother kwa vinywaji.Hatukuw a na ramani yoyote ya kupata kinywaji siku ya leo” alisema yule jamaa

“Kwani ninyi mnajishughulisha na mambo gani? aliuliza Gosu Gosu

“Kazi mbali mbali ukitukodisha tunakufanyia.Sisi ni watu wa kazi,nadhani umenielewa” alisema yule jamaa.

“Nimekuelewa” alisema Gosu Gosu

“Wewe unajishughulisha na nini? Aliuliza yule jamaa

“Mimi pia ninajishughulisha na shughuli kama zenu.” Alijibu Gosu Gosu

“Ouh kumbe wewe ni mwenzetu kabisa.”

“Nataka niulize swali.Kwa nini nimeletwa huku kuja kuifanya hii kazi wakati ninyi mpo? Aliuliza Gosu Gosu

“Siwezi kujua kwa nini.Yawezekana mwenzetu ni mjuzi zaidi kutuzidi” alijibu yule jamaa

“Kazi ni ile ile moja.Kwa mfano yule jamaa niliyemuondoa jana mtu yeyote angeweza kumuondoa.”

‘Simfahamu huyo mtu ni nani.Yawezekana iko sababu kwa nini ukaletwa wewe kumuondoa”

“Kwa nini humfahamu? Jombaa hajakueleza kitu chochote kuhusiana na yule mtu?

“Hapana hajanieleza chochote kuhusiana na kazi uliyokuja kuifanya.”

“Kwa nini? Ninyi si timu moja? Kwa nini asiwaeleze kile kinachoendelea? Aliuliza Gosu Gosu

“Alitueleza kwa kifupi tu kuwa umekuja hapa kufanya usafi.Hili ni neno tunalolitumia tukimaanisha kumuondoa mtu duniani ila hakutueleza kwa undani ni akina nani unaokuja kuwaondoa”

“Unawafahamu watu walionieleta hapa kuja kufanya usafi? Aliuliza Gosu Gosu

“Hapana.Jombaa ndiye kiongozi wetu.Yeye ndiye hupokea kazi kutoka kwa watu mbali mbali halafu anatupangia nini cha

kufanya.Hatuhoji kazi imetoka kwa nani.Sisi tukielekezwa kuua mtu au kufanya chochote tunafanya.” alisema yule jamaa

“Unaionaje kazi hii inakulipa? Aliuliza Gosu Gosu

“Ina malipo mazuri lakini tunaweza kuchukua hata miezi kadhaa hatujapata kazi ya kufanya hivyo tunakuwa katika wakati mgumu sana ila tukizipata zinakuwa ni fedha nyingi” alijibu

“Kuna mtu natakiwa kumuondoa kesho.Unaweza

ukawa na fununu ni nani? Aliuliza Gosu Gosu

“Hajakwambia Jombaa ni nani unayekwenda kummaliza?

“Hapana hajanieleza chochote”

“Hata sisi hatufahamu chochote.Usiwe na hofu atakueleza hata hiyo kesho.Jombaa huwa hakurupuki ni mtu wa mipango mikubwa” alijibu yule jamaa na mara ikasikika honi ya gari akatoka nje akaenda kufungua geti.Yule jamaa

aliyekwenda kuleta vinywaji alirejea.Vinywaji viliwekwa mezani.

Jombaa alirejea saa nane usiku ,aliwakuta vijana wake wamelewa chakari.Alishangaa kumkuta Gosu Gosu sebuleni

“Ulisema hutarudi leo.Imekuaje? aliuliza Jombaa huku akiwasha sigara

“Nimeamua kurudi.Nilikumbuka kesho nina kazi hivyo sikutaka kujichosha nikarejea nikaagiza vinywaji tukanywa hapa hapa nyumbani.” Alijibu Gosu Gosu

“Hakuna tatizo hata kama ungelala kwani kazi itakuwa usiku wa kesho” alisema Jombaa

“Unaweza ukanidokeza ni nani ninayekwenda kumuondoa hiyo kesho? Gosu Gosu aliuliza

“Utamfahamu hiyo kesho usihofu” alijibu Jombaa akawasaidia vijana wake kuinuka kwenda kulala.

****

Jiji la Arusha liliamshwa na hali ya ubaridi kama ilivyo kawaida yake.Saa kumi na mbili na nusu Mathew Mulumbi aliamka akafunua pazia akachungulia nje.Tayari barabara nyingi za jiji la Arusha zilikwisha jaa magari watu wakielekea katika shughuli mbali mbali za kila siku.

“Ninalipenda hili jiji hasa hali yake ya hewa.” Aliwaza akaingia bafuni akaoga halafu

akamfuata Ruby chumbani kwake

“Uko salama kabisa? Aliuliza Mathew

“Niko salama kabisa” alijibu Ruby

“Kuna chochote umefanikiwa kukipata kuhusiana na Regina? Mathew aliuliza

“Niliwasiliana na rafiki yangu mmoja nikamtaka anisaidie kupata namba ya simu ya Regina.Aliniunganisha na rafiki yake mwingine

akanihoji maswali kadhaa nikamdanganya kwamba mimi ni mkereketwa wa chama cha ukombozi wa Afrika. Nilimdanganya kuwa ninataka kuchangia kampeni za chama.Alinitaka nitume mchango huo kwa katibu mkuu wa chama nikamwambia nataka kuupitisha kwa naibu katibu mkuu.Alinielewa akanipa namba ya Regina." Alisema Ruby akampa Mathew kijikaratasi alichoandika namba ya simu ya Regina

"Baada ya kuipata namba yake ya simu hakuna kupoteza

muda.Tumpigie simu ili tujue kama bado yuko hapa Arusha ili tufanye mpango wa kuonana naye” alisema Mathew

“Nitatumia simu hiyo vile vile kujua mahali alipo hivi sasa ili iwe rahisi kwetu kumfuatilia endapo kutakuwa na ugumu katika kuonana naye” alisema Ruby na kuweka tayari program zake katika kompyuta halafu akachukua moja ya laini yake ya simu ambayo huitumia kwa shughuli kama hizi iliyosajiliwa kwa jina la Secilia

Mdaki akaiweka katika simu akapiga ile namba ya Regina ikaita.Baada ya muda ikapokelewa

“Hallow” ilisema sauti ya mwanamke upande wa pili wa simu

“Hallow dada habari za asubuhi”alisema Ruby

“Nzuri dada,habari yako”

“Salama kabisa.Naamini nazungumza na mheshimiwa Regina”

“Ndiyo.Nani mwenzangu?

“Mimi naitwa Secilia Mdaki ni mfanyabiashara na mkereketwa wa chama cha Ukombozi wa Afrika”

“Ahsante sana.Uko wapi dada Secilia? Aliuliza Regina

“Niko Dar es salaam.Wewe uko wapi kwa sasa?

“Kwa sasa niko Arusha”

“Dada nina mchango wangu ambao nimejichanga na wenzangu wachache kwa ajili ya kugharamia kampeni . Nilidhani uko Dar es salaam nije nikukabidhi”Alisema Ruby

“Nenda kaukabidhji mchango huo katika ofisi kuu ya chama jijini Dar es salaam.Pale utaonana na katibu mkuu au wahusika wengine wa chama wataupokea” alisema Regina

“Ahsante sana dada lakini nilihitaji sana nikukabidhi mchango wewe mwenyewe kwa sababu kuna mambo nilitaka tuzungumze.Hata hivyo utakaporejea Dar es salaam unijulishe ili tuonane lakini mchango nitaukabidhi katika makao makuu ya chama

hapa Dar es salaam” alisema Ruby

“Nashukuru sana dada Secilia.Nitakutafuta nitakaporejea Dar es salaam ili tuonanane na unieleze suala lako.Ahsante kwa kutuunga mkono” alisema Regina

“Nitashukuru sasa dada Regina.By the way nimefurahishwa sana na kazi yako.Hongera sana.Unahamasisha wanawake wengi waingie katika siasa”

“Ninashukuru sana dada.Uwe na siku njema” alisema Regina akakata simu.

“Bado yuko hapa Arusha.Amenielekza michango yangu niipeleke katika ofisi yao kuu Dar es salaam” Ruby alimwambia Mathew

“Umefanya vyema kutokuwa king’ang’anizi kwa sababu kama ungeng’ang’ania kuonana naye angepata wasi wasi.Kwa sasa tujue mahali alipo.Progamu imefanikiwa kujua mahali alipo? Aliuliza

Mathew.Ruby alicheza na kompyuta yake kwa muda.

“Programu inaonesha yuko hapa” alisema Ruby na kumuonesha Mathew mahali katika ramani ya jiji la Arusha ambako kulikuwa na mduara mdogo mwekundu.

“Ngaramtoni.Tutakwenda mahali hapo kumtafuta.Hata hivyo nina wazo lingine.Baadae saa tano hivi utampigia tena simu utamjulisha kuwa umempata mtu anayekuja Arusha.Utamuuliza kama

itawezekana umpe mchango wako huyo mtu amletee.Lengo hapa ni kujua mahali alipo muda huo na vile vile kujaribu kutafuta tena nafasi ya kuonana naye” alisema Mathew

“Ni wazo zuri sana hilo” alisema Ruby

“Vile vile tutahitaji kupata gari ambalo tutalitumia katika mizunguko yetu mbali mbali tukiwa hapa Arusha.Hilo si tatizo kwani yapo makampuni yanayokodisha magari hapa Arusha.Vile vile itatulazimu

kupata nyumba hata kama ni kwa siku chache kwa sababu hatuwezi kufanyia kazi zetu hapa hotelini si salama sana.Tutazungumza na madalali wa nyumba ili watutafutie nyumba ya kukodi.Ninapenda sana eneo la Njiro kule kumetulia ” alisema Mathew

****

Gosu Gosu aliamka mapema sana asubuhi akaenda nyuma ya nyumba ambako kulikuwa na vyuma

vya kufanyia mazoezi.Jombaa alifika akaungana naye katika mazoezi.Saa mbili za asubuhi walipumzika

“Kuna taarifa yoyote kuhusiana na muda au mahali ambako shughuli itafanyika? aliuliza Gosu Gosu

“Usiwe na hofu kaka muda utakapowadia utajulishwa”alijibu Jombaa

“Sipendi kushtukizwa.Ninapenda kuelezwa mapema kazi ninayoptakiwa kuifanya ili nijiandae” alisema Gosu Gosu

“Vuta subira kila kitu kitakwenda vizuri” alisema Jombaa kila mmoja akaelekea katika chumba chake.Baada ya kuoga Gosu Gosu alijumuika na wengine kupata kifungua kinywa.Baada ya kupata kifungua kinywa Jombaa na watu wake waliingia garini bila kumueleza Gous Gosu wanakwenda wapi.Gosu Gosu alirejea chumbani kwake akajifungia chumbani na kwa kutumia ile saa yenye laini ya simu akampigia simu Mathew

“Gosu Gosu unaendelaje?

“Ninaendelea vyema.Vipi ninyi mko salama?

“Tuko salama.Kuna habari mpya?

“Nimepiga kuwajulia hali.Wale jamaa nimewachimba kwa undani sana hata wenyewe hawafahamu chochote kuhusiana na kazi ya leo.Hawa jamaa wanafanya kazi ya kukodishwa kama vile ujambazi,mauaji,wizi wa magari n.k.”

“Ahsante kwa taarifa hiyo Gosu Gosu.Kwa upande wetu

tumekwisha pata namba ya simu ya Regina tumewasiliana naye tukagundua kwa asubuhi hii yuko eneo la Ngaramtoni hapa Arusha .Hatujui kama huko ndiko anakoishi au yuko huko kwa muda tunaendelea kufuatilia.” Alisema Mathew na kumweleza Gosu Gosu mikakati yao yote ya siku ile

****

Hadi ilipofika saa sita mchana,tayari Mathew na Ruby walikwisha pata gari la kukodi kwa ajili ya kuwasaidia

katika mizunguko yao jijini Arusha.Tayari vile vile walikwisha onana na dalali wa nyumba wakampa kazi ya kuwatafutia nyumba maeneo ya Njiro au kwingine kokote kwenye utulivu wa kutosha. Baada ya kukamilisha mambo hayo mawili walishika njia kuelekea Ngaramtoni mahali ambako ilionesha ndiko alikokuwa Regina asubuhi.

Ruby ambaye alikuwa pembeni akiifuatilia ramani ile ili kujua mahali alikokuwa Regina wakati alipozungumza naye asubuhi alimpa

maelekezo Mathew na wakajikuta wametokea katika nyumba moja kubwa ya ghorofa mbili.Nje ya nyumba ile kulikuwa na walinzi wawili wa kampuni binafsi ya ulinzi.Bendera za chama cha ukomozi wa Afrika zilipepea katika ile nyumba

“Ramani inatuelekeza wakati Regina anapokea simu asubuhi alikuwa hapa” alisema Ruby huku wakilitazma jumba lile

“Je hapa ndipo anapoishi? Mbona inaonesha hapa ni

kama ofisi ya chama?Aliuliza Mathew.

Gari walimokuwamo lilikuwa na vioo vyeusi hivyo haikuwa rahisi kwa wao kuonekana kirahisi.Wakiwa wanaendelea kufanya uchunguzi magari mawili yenye bendera za chama cha Ukombozi

“Nyumba hii inaonesha inatumiwa na chama cha ukombozi.Inawezekana hii ni moja ya kambi zao au mahali wanakoishi viongozi.” Alisema Ruby

“Inaonekana hivyo.Lakini hebu mpigie simu kwa mara nyingine tena umpe ile taarifa niliyokwambia ili tufahamu kama yuko humu ndani au vipi.” Alisema Mathew.Ruby alimpigia tena simu Regina.Simu iliita bila kupokelewa akapiga tena ikapokelewa

“Hallow” ilisema sauti ya Regina

“Dada Regina ni mimi Secilia nilikupigia asubuhi,samahani tena kwa usumbufu.”

“Bila samahani.Unasemaje dada?

“Nimempata rafiki yangu mmoja ambaye anakuja Arusha nikaona nikuulize je nimpe huyo ule mzigo akufikishie? Aliuliza Ruby.Zilipita sekunde kadhaa Regina akajibu

“Atafika saa ngapi huku Arusha?

“Anakuja na ndege atafika saa kumi na moja jioni.Nitampa huo mzigo na barua yenye maelezo yangu binafsi ambayo utayasoma

halafu utanishauri nini nifanye.” Alisema Mathew

“Sawa.Utampa namba yangu ili anipigie atakapofika hapa halafu nitamjulisha wapi nitaonana naye”

“Ahsante sana dada.” Alisema Ruby na kukata simu.

“Tumempata.Wewe ndiye utakayejifanya ni rafiki yangu kutoka Dar es salaam ambaye utakwenda kuonana naye baadae jioni” alisema Ruby.Mathew aliwasha gari wakaondoka.

****

Kila kitu walichokihitaji akina Mathew walifanikiwa kukipata.Tayari walifanikiwa kupata nyumba nzuri yenye kila kitu ndani eneo la Njiro Ambayo waliikodisha kwa siku saba.

“Nadhani ni muda muafaka wa kumpigia Regina” alisema Mathew.Akitumia laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina la Festus Mbwela alimpigia simu Regina.

“Hallo” ilisema sauti ya mwanamke

“Hallo dada habari ya jioni”

“Nzuri kaka.Nazungumza na nani? Aliuliza Regina

“Ninaitwa Festus Mbwela.Nimepewa namba yako na dada mmoja anaitwa Secilia yuko Dar es salaam ili nikupigie nifikapo Arusha.Amenipa mzigo wako” alisema Mathew

“Ouh ! Nilikwisha sahau kabisa.Uko wapi kwa sasa? Aliuliza Regina

“Kwa sasa tayari niko hapa Arusha.Sijui kama tunaweza kuonana jioni hii mara moja nikakupa mzigo kwa sababu kesho asubuhi sintakuwa na nafasi nitakuwa na ratiba nyingine” alisema Mathew

“Sawa kaka.Nitakujulisha baada ya muda mfupi wapi tutakutana” alisema Regina akakata simu

“Vipu kuhusu Gosu Gosu? Mbona hatujapata mrejesho wowote kutoka kwake hadi sasa? Aliuliza Mathew

“Kuna kitu hapa nimekigundua.Hawa watu waliomleta huku lazima wamemfuatilia muda mrefu wanafahamu kuwa ana mahusiano na sisi hivyo wako makini sana ili mipango yao isiharibike.Hawataki kumweleza mapema ni nani ambaye anatakiwa kuuawa kuogopa mpango kuvuja.Inawezekana ni mtu mkubwa ndiyo maana wanafanya siri.Tuendelee kuvuta subira tutajua kila kitu” alisema Mathew na kunyamaza baada ya ujumbe

mfupi kuingia katika simu yake akaufungua ulitoka kwa Regina.

“Saa moja na nusu tukutane Duma bar”

“Mambo yameiva.” Alisema Mathew

“Nitaweka katika simu yako program ambayo utakapokuwa karibu na Regina utaiwasha ambayo itaiona simu ya Regina na kuniwezesha mimi kuiunganisha na kompyuta yangu.Tutaweza kufuatilia mazungumzo yake kujua

anawasiliana na akina nani.Lazima ipo sababu kwa nini yule jamaa Anganile bandia alikuwa anamfuatilia.” Alisema Ruby akaichukua simu ya Mathew akaiwekea ile program aliyoisema.Wakati wakijiandaa kuondoka simu ya Mathew ikaita ilikuwa ni Gosu Gosu.

“Gosu Gosu.Tumekusubiri sana.Kuna taarifa yoyote mpya?” aliuliza Mathew

“Mpaka sasa hakuna taarifa yoyote.Wale jamaa hawajarejea tangu

walipoondoka asubuhi.Watakaporejea na kunijulisha kuhusiana na kazi tunayokwenda kuifanya leo nitatafuta namna ya kuwajulisha” alisema Gosu Gosu

“Kuwa makini sana.Sisi tunakwenda kuonana na Regina jioni hii ya leo.Kupita kwake naamini tunaweza kupata mambo ya muhimu kuhusiana na yule Anganile” alisema Mathew.

“Kila la heri Mathew nami nitakapopata chochote

nitawajulisha” alisema Gosu Gosu wakaagana.Akina Mathew waliondoka kuelekea Duma hotel mahali alikoelekeza Regina

****

Tayari giza lilikwisha ingia pale Jombaa na vijana wake waliporejea katika makazi yao tangu walipoondoka asubuhi.

“Umeshindaje hapa? Jombaa alimuuliza Gosu Gosu

“Salama kabisa” alijibu Gosu Gosu

“Jiandae tunakwenda kazini” alisema Jombaa

“Kazi inafanyikia wapi? Naweza kufahamu nani ninayekwenda kumuondoa ili nijiandae? Aliuliza Gosu Gosu

“Usiogope.Jiweke tayari muda mfupi ujao tunaondoka” alisema Jombaa akaufunga mlango wa chumba cha Gosu Gosu akaondoka kuelekea chumbani kwake

“Kwa nini hawa jamaa wamekuwa wasiri sana kuhusu mtu ambaye ninakwenda kumuua usiku wa leo? Au kuna kitu wamegundua kuhusu mimi? Alijiuliza Gosu Gosu

Jamaa walitumia dakika ishirini kujiandaa halafu Gosu Gosu akafuatwa.

“Muda wa kazi” alisema Jombaa.Gosu Gosu hakuuliza kitu aliongozana na Jombaa wakaingia garini wakaondoka. Gosu Gosu alijifanya anatazama saa halafu

akabonyeza kitufe alichoelekezwa.

“Kazi imeanza” alisema Gosu Gosu akiwajulisha akina Mathew

“Umesemaje? Aliuliza Jombaa

“Nasema kazi imeanza” alisema Gosu Gosu

“Kazi ya leo imebadilika kidogo.Inabidi kuwaondoa watu wawili na si mmoja tena.” Alisema Jombaa

“Watu wawili? Aliuliza Gosu Gosu

“Ndiyo.Idadi imeongezeka.” alijibu Jombaa safari ikaendelea kimya kimya bila Gosu Gosu kujua wanakoelekea.

****

Gari la akina Mathew liliwasili Duma bar.Taratibu walielekea katika maegesho.Kabla ya kushuka Mathew alichukua simu akampigia Regina

“Hallo kaka” alisema Regina baada ya kupokea simu

“Dada tayari nimefika hapa katika hii baa uliyonilekeza” alisema Mathew

“Ahsante kwa kujali muda.Njoo upande wa Mashariki karibu na bwawa la kuogelea utaniona nimekaa katika meza peke yangu.” Alisema Regina

“Ahsante ninakuja” alisema Mathew akakata simu.

Alitembea taratibu na kwa tahadhari kubwa akijaribu kuangaza kama kuna hatari.Alifika katika bwawa la kuogelea akasimama akatoa

simu akapiga simu.Upande wake wa kulia alimuona mwanamke mmoja akiinua simu.

“Nadhani ni yule pale” aliwaza Mathew akaiwasha ile programu ambayo Ruby aliiweka katika simu yake.Alitembea taratibu akimfuata yule mwanamke

“Haswa ni yeye” aliwaza alipomkaribia zaidi

“Habari yako dada” alisema Mathew

“Karibu sana kaka’

“Ahsante.” Alijibu Mathew akaketi.

“Ahsante umefika kwa wakati” alisema Regina ambaye aliweka simu mbili mezani

“Ahsante.” Alisema Mathew

“Nilipewa maelekezo na dada mmoja anaitwa Secilia nikuletee mzigo.Sikujua kama mzigo huo ninakuleta wewe.Ninakufahamu wewe ni mtu maarufu uko katika chama cha siasa cha Ukombozi wa Afrika.Tunakufahamu ni

mwanadada mpambanaji” alisema Mathew.Regina alitabasamu

“Ahsante nashukuru” alisema Regina

“Kampeni zinakaribia mmejiandaaje? Aliuliza Mathew

“Tumejiandaa vizuri.Tunatarajia kuzindua kampeni zetu hapa Arusha ndiyo maana nimekuwa hapa Arusha kwa zaidi ya mwezi sasa kufanya maandalizi ya kampeni” alisema Regina

“Ouh sikujua kama kampeni zenu mtazindulia huku Arusha.Lakini nini matarajio yenu katika uchaguzi mkuu ujao? Aliuliza Mathew

“Tumejiandaa vizuri kuingia katika ushindani japokuwa kazi haitakuwa nyepesi.Pamoja na ushindani utakaokuwepo tutajitahidi kunadi sera zetu kwa wananchi ili watuchague tuongoze nchi.Tuna hakika tumeweka wagombea wazuri katika nafasi zote za urais ,ubunge na udiwani.Tunawategemea sana

watu kama ninyi wafanya biashara mtupigie kura ili tuwaletee ukombozi wa kiuchumi kama jina la chama chetu.”alisema Regina

“Kuhusu hilo msiwe na hofu yoyote.Wafanya biashara wengi tuko nyuma yenu.Mmekuwa wasemaji wazuri wa wafanya biashara hivyo basi hatutawatupa.Lazima tuwapigie kura.Binafsi nitawahamasisha wenzangu wote ninaowafahamu ili tukichague chama chenu” alisema Mathew

“Nitashukuru sana kwa msaada huo.Katika uchaguzi huu hata kura moja ina nguvu sana ya kubadili matokeo hivyo kila kura moja ina maana kubwa kwetu.By the way ulisema unaitwa nani? Aliuliza Regina

“Naitwa Festus Mbwela” alijibu Mathew

“Sura hi kama si ngeni kwangu.Ninafikiria nimewahi kuiona wapi kumbu kumbu haiji.Ila nina uhakika kuna sehemu nimewahi kukuona” alisema Regina

“Yawezekana kweli tumewahi kuonana katika harakati mbali mbali za kutafuta mkate wa kila siku.Kama hutajali ninaweza kununua kinywaji? Aliuliza Mathew.Regina alitabasamu na kusema

“Hakuna tatizo” alisema Regina.Mathew aligeuka akanyoosha mkono akamuita muhudumu akamuagiza awaletee vinywaji.Aliufungua mkoba wake akatoa bahasha akampatia Regina.

“Hiyo ni bahasha ambayo nimepewa na Secilia nikuletee”alisema Mathew

“Ni mchango wake kwa kampeni zetu.Nilimtaka aupeleke katika ofisi zetu kuu lakini alisema anataka mchango huu unifikie mimi mwenyewe.Nitampigia simu nimshukuru.Tunahitaji sana michango ya wadau mbali mbali.” Alisema Regina

“Mimi pia nitajitahidi niwasilishe mchango wan.....” alinyamaza Mathew baada ya mtu mwingine kutokea.

“Jamani habari zenu? Alisalimu yule jamaa

“Salama Amani.Karibu sana.Nimepata mgeni jioni hii.Anaitwa Festus anatokea Dar ni mfanya biashara ameniwasilishia mchango kutoka kwa mmoja wa wakereketwa wa chama chetu.Festus huyu ni mwenzangu.Tuko naye katika harakati za chama.Yeye ni dereva wa mwenyekii wa chama.” alisema Regina.Mathew aliinuka akampa mkono Amani wakasalimiana

“Tunashukuru kaka kwa kutuunga mkono katika harakti zetu za ukombozi.” Alisema Amani

“Tutaendelea kuwaunga mkono kwa kila namna hadi tuhakikishe mnashinda uchaguzi huu” alisema Mathew

“Mbona meza haina vinywaji? Aliuliza Amani

“Tumekwisha mua…..” Mathew hakumaliza sentensi yake muhudumu akafika na sinia lenye vinywaji.Amani akamtaka muhudumu akaongeze vinywaji.

“Festus jumuika nasi kwa kinywaji tafadhali” alisema Amani

****

Gari la Jombaa liliwasha taa ya upande wa kulia kuashiria kukata kona na kufuata barabara inayoelekea katika moja ya baa maarufu jijini Arusha Duma bar.Geti lilikuwa wazi wakaingia wakafuata barabara ya upande wa kushoto ambayo ilikwenda hadi nyuma ya jengo lile la baa

ambako kulikuwa na jengo refu la ghorofa

“Hii ni baa maarufu sana hapa Arusha.Watu wengi hupenda kuja hapa kutokana na umaarufu wake hasa nyama choma nzuri .Hili jengo la nyuma ni nyumba ya wageni” Alisema Jombaa.Alifungua mlango akashuka akamtaka Gosu Gosu amfuate.Waliingia ndani ya jengo lile wakapanda lifti hadi ghorofa ya sita wakashuka wakatembea hadi katika chumba ambacho hakikuwa na namba.Jombaa aligonga mlango ukafunguliwa

wakaingia ndani.Mle ndani kulikuwa na watu wanne pamoja na kompyuta zipatazo sita.Katika meza kulikuwa na bunduki mbili za udunguaji zimewekwa tayari.Mmoja wa wale watu alitoka katika meza yake akawafuata akina Jombaa

“Karibuni.Kila kitu kinakwenda vizuri.Tayari wahusika wamekwisha fika.” Alisema yule jamaa

“Huyu niliyeongozana naye ndiye mtendaji mkuu wa shughuli ya leo.” Alisema Jombaa akamtaka Gosu Gosu

kujiandaa.Jombaa na yule jamaa walisogea pembeni.

“Kuna tatizo limejitokeza” alisema yule jamaa

“Tatizo gani?

“Tulitegemea watu wawili ambao tayari wote wamefika lakini amejitokeza mtu mwingine wa tatu ambaye hatumfahamu ni nani.”alisema yule jamaa huku akimuonesha Jombaa picha ya wale jamaa watatu wakiwa mezanio wakipata vinywaji.

“Huyu aliyejitokeza ni bahati mbaya kwake.Tutawaondoa wote” alisema Jombaa.Alichukua kiona mbali akaelekea dirishani.Taa zilzimwa akalifungua dirisha.Kwa kutumia kiona mbali aliweza kuwaona watu wote waliokuwa wamekaa upande wa mbele wa hoteli.Jombaa aligeuka akamtaka Gosu Gosu kuchukua moja ya zile bunduki akamtaka asogee dirishani.

Jombaa akiwa na kiona mbali alimpa maelekezo Gosu Gosu kuhusiana na watu

wanaotakiwa kuondolewa.Gosu Gosu alifuata maelekezo aliyopewa na Jombaa.

“Nimewaona watu hao mbona ni watatu? Aliuliza Gosu Gosu

“Walengwa hapo ni wawili lakini kwa kuwa huyu mmoja amejitokeza naye aondolewe pamoja nao.Tunaanza na yule mwanamke,tafuata yle aliyevaa shati jeupe wa mwisho yule mwenye koti.” Alisema Jombaa

“Makubaliano yangu nanyi yalikuwa kumuondoa mtu mmoja ..” alisema Gosu Gosu na mara alihisi kuguswa na kitu cha baridi kichwani.Alikuwa amewekewa bastola .

“Utafanya kazi au nikufumue kichwa chako sasa hivi? Aliuliza Jombaa ambaye sura yake ilionesha ukatili mkubwa

“Easy bro…..tufanye kazi” alisema Gosu Gosu akiielekeza bunduki katika ile meza yenye watu watatu wanaotakiwa

kuuawa.Kupitia lensi yenye nguvu iliyokuwa juu ya bunduki ile kubwa ya udunguaji aliona kitu kilichomshtua mno.

“Oh my God ! alisema Gosu Gosu kwa sauti ndogo

“Mathew Mulumbi.Anafanya nini pale? Halafu yule mwanamke mbona ni Regina.” Aliwaza Gosu Gosu.Alihisi kutetemeka mikono.

“Uko tayari? Aliuliza Jombaa lakini Gosu Gosu hakujibu kitu

“Uko tayari? Aliuliza tena Jombaa lakini bado Gosu Gosu alikuwa kimya.Jombaa alimsogelea Gosu Gosu.

“Kuna tatizo? Aliuliza

“Hakuna tatizo” alijibu Gosu Gosu

“Nitahesabu hadi tatu kisha utamaliza mchezo.Tunatakiwa kuondoka hapa haraka sana” alisema Jombba.Gosu Gosu aliwashuhudia wale jamaa waliowakuta mle chumbani wakizifunga kompyuta zao tayari kwa kuondoka.

“Moja ! alisema Jombaa

“Siwezi kumuua Mathew Mulumbi wala Regina.Lazima nitafute namna ya kufanya kuwaokoa” aliwaza Gosu Gosu

“Mb…..” alihesabu Jombaa lakini Gosu Gosu hakusubiri Jombaa amalize kuhesabu, aliachia risasi ya kwanza iliyompata Amani shingoni.Kabla hawajakaa sawa aliachia risasi ya pili iliyompata kichwani akaangukia mezani

Kitendo cha Amani kuanguka juu ya meza huku

akivuja damu,kiliwashtua sana akina Mathew.Wakiwa bado wanashangaa, ilipigwa risasi ya tatu ambayo ilizisambaratisha chupa zilizokuwa mezani.Kama kima Mathew Mulumbi alimrukia Regina akamuangusha chini.Alichomoa bastola yake akatazama pande zote kama kuna mtu karibu yao lakini hakukuwa na mtu yeyote mwenye silaha pale karibu

“A sniper” alisema Mathew

“Regina sikiliza kuna mdunguaji yuko sehemu

anatushambulia.Ili tuokoke utafuata kile nitakachokuelekeza” alisema Mathew.Alifungua kiwambo cha bastola yake halafu akaachia risasi mbili hewani.Mlio ule wa risasi ulileta taharuki kubwa watu wakaanza kukimbia hovyo.Mathew akiwa amemshika mkono Regina walitoka mbio wakiungana na watu wengine waliokuwa wanakimbia kunusuru maisha yao

“Umefanya kitu gani? Jombaa aliunguruma kama Simba.Sura yake ilifura hasira

“Haikuwa rahisi kuua watu wote watatu lakini nimeua mmoja.Katika harak……..” Gosu Gosu alijitetea lakini ghafla akapigwa na kitu kizito akaanguka chini.

“Umeharibu misheni nzima.” alisema Jombaa


MAMBO AMEANZA.

USIKOSE SEHEMU IJAYO…

NI HIVI KARIBUNI.

USIKOSE KITABU HIKI KUFAHAMU BALAA LA MATHEW MULUMBI AKISHIRIKIANA NA GOSU GOSU,RUBY NA AGAI SEMPA.

WEKA ODA YAKO MAPEMA



ULIIFURAHIA SIMULIZI HII KATIKA NAKALA TETE?

HIVI KARIBUNI ITAKUJIA IKIWA IMEBORESHWA KATIKA NAKALA NGUMU (HARDCOPY)

